## Contents

UTANGULIZI .......... 9

KUANZA .......... 12

SOMO LA KWANZA SEHEMU111 .......... 14

UTANGULIZI .......... 14

SWALI: Mwanzo 1:1 inatwambia? .......... 15

SWALI: .......... 16

SWALI: .......... 16

SALA: .......... 17

SOMO LA KWANZA~~~ SEHEMU YA 222 .......... 17

Soma Mwanzo1. .......... 17

ZOEZI: .......... 18

ZOEZI: .......... 19

SWALI: Tunajifunza nini kuhusu Mungu kutokana na mistari hii ya mfano? .......... 19

MASWALI YA KUTAFAKARI: .......... 20

KUCHIMBA KWA KINA: .......... 20

SWALI LA KUTAFAKARI: .......... 21

SALA: .......... 21

SOMO LA NNE~~~ SEHEMU YA333 .......... 21

SWALI: .......... 22

FUNDISHO: .......... 22

ZOEZI: .......... 23

MATUMIZI YA ZOEZI: .......... 24

SALA: 24

SOMO LA KWANZA~~~SEHEMU YA 444 25

ZOEZI: 25

Kutoka Mwanzo 1: 25

Kutoka Mwanzo 2: 26

FUDISHO: 27

MASWALI YA KUTAFAKARI: 27

KUCHIMBA KWA KINA: 28

SALA: 29

SOMO LA KWANZA~~~ SEHEMU YA555 29

FUNDISHO: 29

SWALI: 30

KUCHIMBA KWA KINA: 30

MARUDIO: 31

SWALI: 31

SWALI LA KUTAFAKARI: 32

SOMO LA PILI~~~ SEHEMU YA111 33

UTANGULIZI: 33

Zoezi: 33

KUKARIRI: 34

SOMO LA PILI~~~ SEHEMU YA 222 35

FUNDISHO: 35

MASWALI: 35

KUCHIMBA KWA KINA: 37

MATUMIZI: 37
SALA: 39
SOMO LA PILI~~~SEHEMU YA 333 39
FUNDISHO: 39
KUTAFAKARI: 41
MATUMIZI: 42
SALA: 43
FUNDISHO: 43
SWALI LA KUTAFAKARI: 44
SWALI LA KUTAFAKARI: 45
SWALI LA KUTAFAKARI: 46
KUKARIRI: 47
UFAFANUZI: 47
SALA: 48
SOMO LA PILI ~~~ SEHEMU YA 555 49
MATOKEO #1: 50
MATOKEO #2: 50
SWALI: 51
MATOKEO #3: 52
REFLECTION: 53
SALA: 53
SOMO LA TATU ~~~ SEHEMU YA 11 54
UTANGULIZI: 54
FUNDISHO: 55

KUCHIMBA KWA KINA: 56
KUKARIRI: 57
SOMO LA TATU ~~~ SEHEMU YA 222 57
ZOEZI: 57
FUNDISHO: 58
MAZOEZI: 59
MASWALI YA KUTAFAKARI: 60
SALA: 61
MAWAZO YA KUFUNGA SEHEMU YA 2: 61
SOMO LA TATU ~~~SEHEMU YA 333 62
UTANGULIZI: 62
ZOEZI: 63
FUNDISHO: 64
SOMO LA TATU ~~~ SEHEMU YA 444 65
ZOEZI: 65
SOMO LA TATU ~~~SEHEMU YA 555 70
KUCHIMBA KWA KINA: 71
➢ MAFAFANUZI: 72
MASWALI YA MATUMIZI: 73
SALA: 74
MASWALI: 75
ZOEZI: 75
MASWALI: 76
SOMO LA NNE ~~~ SEHEMU YA 222 77

UTANGULIZI: 77
ZOEZI: 77
MASWALI: 78
TAFAKARI: 79
MASWALI YA MATUMIZI: 80
SALA: 80
SOMO LA NNE~~~ SEHEMU YA 333 80
MASWALI: 81
ZOEZI: 83
MATUMIZI: 83
KUCHIMBA KWA KINA: 84
SALA: 85
MASWALI: 85
TAFAKARI: 86
SALA: 89
SOMO LA NNE~~~ SEHEMU YA 555 89
UTANGULIZI: 89
MASWALI: 90
KUKARIRI: 91
FUNDISHO: 91
➢ *MAANA: Huruma* ina maana kuwa Mungu hakuamua kutufanyia kama itustahilivyo. Kutokana na dhambi zetu na hali a mioyo yetu ya kutenda dhambi, tunastahili kuadhibiwa na kufa. Katika Warumi 6:24 mshahara wa dhambi ni *mauti* lakini karama ya Mungu ni *uzima wa milele* katika Kristo Yesu Bwana wetu. Tunacho stahili ni kifo, lakini Mungu anatuonyesha Huruma yake kwa kutupatia kile tunachostahili.Badala yake, Anaonyesha upendo wake kwetu kwa kutupatia uzima wa milele katika Yesu. 91

MATUMIZI: 91

SALA: 93

KUTAFAKARI: 93

SOMO LA TANO~~~SEHEMU YA 11 94

UTANGULIZI: 94

MASWALI: 95

SALA: 96

SOMO LA TANO ~~~ SEHEMU YA222 97

UTANGULIZI: 97

KUCHIMBA KWA KINA: Soma Mambo ya Walawi17:10-14. 97

➢ *MAANA*: *Dhabihu/sadaka* – Kutoa dhabihu kwa ajili ya dhambi za wanadamu ilimaanisha hakukuwa tena na chochote cha kuzuia au kuingilia uhusiano kati ya Mungu na mwanadamu. Ilimaanisha kuwa *walikuwa katika umoja* na Mungu. Damu liyomwagika ilichukuliwa kama sadaka ambayo ingeondoa dhambi za watu na kugeuza hasira ya Mungu. Mungu alisamehe dhambi za watu walipo mwaga damu ya wanyama na kumtolea sadaka. 98

KARIRI: 99

SALA: 99

SOMO LA TANO ~~~ SEHEMU YA 333 100

UTANGULIZI: 100

KUCHIMBA KWA KINA: 101

KUTAFAKARI: 102

SALA: 103

SOMO LA TANO ~~~SEHEMJU YA 444 104

FUNDISHO: 104

MASWALI YA KUTAFAKARI NA MATUMIZI: 104

SALA: ..... 106

SOMO LA TANO~~~ SEHEMU YA555 ..... 107

MARUDIO: ..... 107

MARUDIO YA MAFUNDISHO: ..... 107

SALA: ..... 109

SOMO LAIIIX ~~~ SEHEMU YA111 ..... 110

FUNDISHO: ..... 110

➢ *MAFAFANUZI: Agano* – Ni makubaliano yaliyoanzishwa na upande mmoja na kutolewa kwa upande wa pili. Agano huendelea kuwapo hadi upande mmojawapo huivunja au huacha mapatano. *Kumbuka:*Unaweza kuwa umezoea agano. Mfano, ukienda benki kwaajili ya kupata mkopo, benki huwa na wakala wa kuweka makubaliano kufuatana na mkopo na mkataba kwako mkopaji.Pande mbili zikisha saini, agano huwa walaka halali ambao utatumiwa kisheria. Kuhusiana na hali hii, Mungu aliazisha ahadi ya huruma yake. Ni ahadi ambayo anafanya,na hawezi kuivunja. Mungu anaimarisha agano na nani? (Mw10)..... 110

MATUMIZI: ..... 112

SALA: ..... 113

SOMO LA IIIX ~~~ SEHEMU YA222 ..... 114

UTANGULIZI:..... 114

MATUMIZI: ..... 116

SALA: ..... 117

SOMO LAIIIX ~~~ SEHEMU YA 333 ..... 118

MATUMIZI: ..... 121

SALA: ..... 122

SALA: ..... 123

SOMO LA IIIX ~~~SEHEMU YA 444 ..... 123

FUNDISHO: ..... 123

MASWALI: .......... 124
FUNDISHO: .......... 125
Rejea Mungu alitaka nini… .......... 126
MATUMIZI: .......... 127
SALA: .......... 128
ZOEZI: .......... 129
FUNDISHO: .......... 129
MATUMIZI: .......... 131
SALA: .......... 132
MARUDIO .......... 132

©FullValue Ministries 2008 1 www.FullValue.org

**MPANGO WA MUNGU CHAGUO LETU**

***ZIARA KATIKA MOYO WA MUNGU***

BY JACKIE OESCH

**"NIMELIFICHA NENO LAKO MONI MWANGU…"**

**ZABURI 119:11**

Maandiko yamechukuliwa toka BIBLIA TAKATIFU, UNION VERSION ®. Copyright © 1997
By Bible Society.of Tanzania. All rights reserved.

***GOD'S PLAN, OUR CHOICE***

## UTANGULIZI

Mwanzo ni kitabu cha mianzo. Mwanzo ina maana ya kuanza. Kitabu hiki cha kwanza hutoa maelezo juu ya uumbaji na huanza na maneno "hapo mwanzo" Katika sura na mistari inayo fuata, tunajifunza juu ya uumbaji wa binadamu wa kwanza, Adamu na mwanamke wa kwanza Eva, na mwanzo wa maisha ya ndoa. Mara moja tunaambiwa juu ya maisha ya kuto tii kwao,maisha ya kuvunja uhusiano wao na Mungu, kuvunja uhusiano wao kwa wao, nafsi zao na hata uumbaji kwa ujumla. Aidha, Mwanzo inasimulia juu ya mpango wa Mungu na ahadi yake ya kurejesha yale yote yaliyo haribiwa na dhaambi. Maana ya neno "Mwanzo" ina jumuisha na mwanzo wa maendeleo ya sayansi na tekinolojia, mwanzo wa lugha, mwanzo mpya ambao Mungu alianzisha na Nuhu baada ya gharika. Kwa nyongeza ni kwamba, habari ya ukoo

wa Adamu, Nuhu, na Shemu iliyoandikwa, inat uunganisha toka mwanzo hadi vizazi vyao vyote vilivyofuata. Sura hii ya somo, huunganisha mianzo mingi ambayo inaonekana katika sura kumi na moja za kwanza.
Kuna mwanzo ulio tajwa katika 2:10 kama jambo la kawaida. Hii ina tukumbusha kuwa, mianzo ya kitabu cha mwanzo si lazima kuwa imetajwa wazi kwenye kitabu hicho. Kipekee kwa jambo hili, mwanzo ni mto. Mstari wa kumi unaanza hivi, mto wa kuimwagilia maji bustani, ulitiririka toka Edeni". Mto huu ambao uligawanyika katika matawi manne, unaweza kuachwa bila kutiliwa maanani, kana kwamba una nafasi ndogo au hauna kabisa katika kujifunza Biblia. Tuna fahamu kuwa kila mto una chanzo. Mto Nile ambao hulisha nchi za Kaskazini mwa Afrika chanzo chake ni Ziwa Victoria. Na kabla ya kuingia Ziwa Victoria huitwa Mto Kagera ambao huanzia kwenye milima ya Rwanda. Mto mkubwa Missisipi hutiririka kupitia New Orleans kuishia kwenye penusula ya Mekisko, chanzo chake ni milima ya Menesota. Yote ina vyanzo pasipo kujali ni mwembamba kiasi gani. Mto huu ambao ulitiririka kutoka Bustani ya Edeni katika hali ya picha, inaonyesha kuwa tayari ulikuwapo katika sura ya pili ya Mwanzo, inaendelea katika historia nzima ya Biblia, hadi sasa na hata milele utakuwapo.

Kwa ufupi tunaweza kufuatilia mto huu kupitia Maandiko katika mistari iliyoorodheshwa hapo chini; ikikumbusha mto huu kama mto harisi na kama mto kwa lugha ya picha, kama mto unao unganisha watu katika historia nzima kwenda kwa yule ambaye ni mwanzo wa uhai wote. Kwa kutumia kalamu ya kuweka alama na daftari, chukua muda na kufanya rejea ya mistari hii. Zingatia lugha ya picha ambazo hujitokea katika masomo yote. Kwa ngazi hii si lazima kuelewa habari zote lakini kwa picha ya maji, mto na mto inakuwa ni ujumbe unaweza kufuatilia.

- Mwanzo 2:10-14
- Hesabu 24:6
- Zaburi 1:3

- 58:11
- Ezekiel 47:5-12
- Yohan 4:13-14
- Yohana 7:37-38
- Ufunuo wa Yohana 22:1

Rejea ulizomaliza kusoma, zinaonyesha kuwa mto ulioanzia Mwanzo 2, inaonyesha kuwa unaendelea kutiririka Biblia nzima hadi Kitabu cha mwisho yaani Ufunuo wa Yohana. Hii picha ya mto wa ukombozi ulifanya Neno la Mungu kuwa sehemu muhimu kwenye maisha ya watu wa Mungu. Mto unao anzia katika Mwanzo, ni mto ambao wana wa Israel waliweka kambi yao kando kando yake, walipokuwa wakizunguka jangwani, kabla ya kuingia katika nchi ya ahadi yaani Kanaani.

Kutoka kwenye maji, walipata mahitaji muhimu, chakula walichohiaji ili waendelee na safari kupitia maisha ya jangwani sawa na Mungu alivyowaelekeza. Katika zaburi ya kwanza, mwandishi wa Zaburi anatufundisha kuwa wale walioishi karibu na maji watakuwa wenye nguvu na kuishi maisha yenye kuzaa matunda. Nabii Isaya kwenye kitabu chake anatumia mfano wa bustani iliyomwagiliwa vizuri maji, kuwa ni kama chemichemi isiyo nyauka.

Picha ya mto inaonekana kupitia historia nzima ya wana wa Israel. Katika kitabu cha Ezekieli, nabii Ezekiel anaandika kuwa mto unatiririka chini ya lango la Hekalu, na anasema kuwa popote mto unakotiririka kuwa kila kitu kitapata uhai. Mwandishi wa kitabu cha Yohana, anatupeleka katika Agano Jipya na analinganisha na yale Yesu aliyosema katika sura ya 4 ya Yohana kuwa atakaye kunywa maji yale ayatoayo hatapata kiu kamwe. Na katika Yohana 7 tunajifunza kuwa Yesu ndiye maji ya uzima na kwa kumwamini tutakuwa na chemichemi ya maji ikibubujika kutoka ndani mwetu.

Mwisho tunamaliza kitabu cha Ufunuo kikiturejesha kwenye picha ya Bustani ya Edeni na kinatupatia picha ya mwisho ya mto unaotiririka kweye ufalme wa mbinguni ambao Yesu ni mtawala kama Bwana na sadaka ya bure “zawadi ya bure ya maji ya uzima”.  Kitabu cha Mwanzo ni kitabu ambacho ni kama kichwa cha maji haya makuu. Utafurahia katika mwanzo wa kupeleleza mwanzo, ulipatikana hapa, kama utakavyojifunza katia hatua yoyote utakayofikia, katika kujifunza Neno la Mungu. Furahia uzoefu. Ninakuombea kuwa, masomo haya yawe chemichemi ya maji ya uzima yatakayo ondoa kiu ya nafsi yako.

## KUANZA

Unarudi kwenye safari ambayo itarekebisha maisha yako yaliyo salia. Safari yako itakuwa ya kipekee kwako.  Kwa sehemu kubwa itategemeana na utayari wako na upendo wako katika kukua kwako katika kuelewa Kitabu hiki, Biblia. Kujitoa kwako kwaajiri ya masomo, kunaashiria kuendelea kwa maisha yako kama vile Mungu anavyo kwambia katika Neno lake. Unahimizwa kuwa na vitu vinne katika mikono yako. Hivi vitu vitakuwa rejea yako katika kujifunza kwako. Utavitumia kila siku katika kuendeleza kujifunza, na katika kupata uzoefu:

1. Nakala ya somo hili la Biblia :*Mpango wa Mungu, Chaguo letu*
2. Toleo la Biblia la Union Version (UV). Kumbuka: Kama unanunua

Biblia mpya, angalia Biblia ambayo ina yafuatayo:

a. Orodha ya Yaliyomo,
b. Iwe na mistari ya rejea upandeni au chini,
c.Itifaki ya Biblia, na
d.ramani chache za msingi.

3. Kalamu au kuandika au kuwekaea alama
4. Daftari au kijitabu cha kuandikia

Kwa vifaa vilivyoorodheshwa hapo juu utakuwa umejiandaa ipasavyo kwa kujifunza na uwe tayari kwa mafanikio katika kutembelea Maandiko. Wakati wa kununua Biblia usikose kuomba ushauri wa muuzaji ili akusaidie, hasa pale unapotafuta Biblia yenye mistari ya rejea.

Usisite kuweka alama kwenye Biblia yako. Unaruhusa! Ndiyo maana kalamu ya kuandikia na ya kuweka alma imo kwenye orodha. Biblia yako ni kwajiri ya kujifunza. Itumie kuandika na kupigilia mistari, kuweka alama, kuzungushia na kuweka miare!Unatishauriwa kutumia daftari yako kuandika kumbukumbu za mawazo yako, maswali, na maendeleo ya safari yako ya kujifunza. Masomo yamegawanyika katika sehemu tano. Vifungu hivi ni mwongozo kukusaidia kuendelea na masomo matika utaratibu mzuri. Kasi ya kujifunza kwako juu yako.

Wakati mwingine somo linaweza kuhitaji muda mwingi zaidi ya ulio nao; kwahiyo itakupasa umalize somo kwa muda zaidi ya ulivyopanga. Wakati mwingine unaweza kumaliza sehemu ya  somo moja na kuchagua kuendelea na somo linalofuata.

Ikiwa hii ni mara yako ya kwanza kujaribu kusoma Biblia, unashauriwa kuanza na somo lenye kichwa cha somo *Kuifanya Biblia Kuwa Yako.* Ni somo ambalo linakupatia zana za kusafiri nazo kukuwezesha kuzunguka Biblia kwa urahisi. *Kuifanya Biblia Kuwa Yako* inaweza kupatikana kwenye mtandao kwa anwani ya
www.FullValue.org.

Japokuwa somo hili linashauriwa  si lazima kwa kufanikiwa katika kujifunza mpango wa *Mungu, Chaguo Letu.* Mwisho,  inabidi ufahamu limeandikwa ili iweze kuwa tayari kujifunza wewe mwenyewe. Imetengenezwa kutumiwa kirafiki, kwa kiwango fulani cha nidhamu ya

mtu mwenyewe. Kwa namna hiyo utamaliza masomo pasipo ugumu wowote. Wakati huohuoa somo litakuwa linavutia, na utakuwa unapata habari mpya. Utahitaji kushirikisha wengine juu ya elimu yako mpya, na utauliza baadhi ya maswali ambayo yataleta changamoto na kutaka majibu. Wakati ukisubiri mambo haya yote, unahimizwa kukaribisha wana ndoa ambao ni marifiki zako ili ushirikiane nao katika kujifunza. Na baadae, wewe na mwezi wako mnaweza kuhitaji wanandoa zaidi ili mjiunge nao. Aidha inaweza kukaribisha rafiki zako ambao ni majirani hata wafanya kazi wenzako.

Labda unafahamu kuwa kanisani kwako kuna ukumbi abao mnaweza kuutumia kujadiliana juu ya masomo yenu ya juma zima. Jaribu kutumia fursa yoyote iliyo salama itakayo wawezesha vikundi vidogo vidogo kukutana mara moja kwa juma kujadiliana juu ya mambo yatakayo wawezesha kukua pamoja kama marafiki katika kuifahamu Biblia. Kila mmoja kwenye kikundi chenu cha kujifunza hata kikiwa kikubwa au kidogo, atakuwa wa msaada kwa kikundi, iwapo mtamwezesha kufanya hivyo!. Ni wakati wa kumpa nafasi mmoja mmoja kuanza!

Fungua Biblia yako kwenye Mwanzo 1. Hebu tuaze na mstari wa kwanza wa sura ya kwanza. Andika maneno matatu ya kwanza;

## SOMO LA KWANZA SEHEMU 11

### *UTANGULIZI*

Watu wengine hawajasoma habari kuhusu uumbaji kama ilivyoandikwa katika sura mbili za Mwanzo. Ikiwa wewe uliisha fanya hivyo, basi siku zote za somo hili zitakuwa ni marudio. Lakini, kama bado, basi utakuwa ni uzoefu wako wa kwanza. Somo hili litakupatia fursa ya kutazama kwa karibu kuhusiana na Biblia inayosema. Makusudi ya somo siyo kujadiliana tu, bali ni kuleta maswali ambayo yatakuongoza kupitia

masomo yatakayo kupatia habari kuhusiana na, ni nini Neno la Mungu lisemavyo, kuhusiana na uumbaji wa mbingu na dunia. Basi furahia kujifunza kwako!

Kwa kuanzia soma sura mbili za kitabu cha Mwanzo.  1 na 2.

.

**SWALI: Mwanzo  1:1 inatwambia?**

1. ________________________________________________________________________

2. ________________________________________________________________________

Mungu ni mwumbaji, mbingu na nchi ziliumbwa. Hebu kwanza tufikirie juu ya uumbaji.

Ukweli ni kwamba Mungu ni mwumbaji. Zilizo orodheshwa hapa chini ni nyongeza za rejea tatu, ambazo hurudia ukweli kuwa ni Mungu aliyeumba:

• Zaburi 102:25 huongea juu ya Mungu na kusema, "____________________________________________________________ ____________________________________________________________________"

• Zaburi 115:15 pia huthibitisha kuwa Mungu ni "____________________________________________________________________"

• Zaburi 148:5 (NIV) husema, "Yeye ________________________________ na  walikuwa

________________________________________________________________________________
_______”

Kwenye daftari yako anza kuandika baadhi ya mawazo yako kuhusiana na, ina maana gani kwako kusema kuwa Mungu ni muumbaji. Fikiria kwa muda kitu fulani ulichoumba. Labda ni mandazi au midoli ya ndege ulaya. Wewe kama uliyekuwa ukiumba, bila shaka ulifanya kazi kwa makini na ulijali sana kazi hiyo. Chukua muda mfupi kutafakari Mungu akiwa kazini, Soma ili kuanza kazi yake ya uumbaji wa mbingu na dunia. Sasa soma Mwanzo1:1-2.

**SWALI:**

Biblia inasema dunia iliumbwa "mwanzo" kabla", Mungu aliumba mbingu na dunia?" (Mwanzo1:1, 2):

________________________________________________________________________________
___

________________________________________________________________________________
___

________________________________________________________________________________
___

Utupu, bila kitu na giza limefunika kila mahali… Inasikia kama miujiza,haikuwa hivyo? Si vigumu kuelewa tupu na giza, lakini maana ya bila umbo ni nini? Tafsiri nyingine huongelea juu ya mwanzo kama wakati wa bila mpangilio na pasipokuwa na kitu, bila umbo na pasipokuwa na thamani. Mwingine huwa na hisia kuwa ilikuwa mchanganyiko na fujo. Wakati fulani wa fujo, pasipokuwa na mpangilio, na utupu Mungu aliamua kufanya kitu.

**SWALI:**

Ni maneno gani katika Mwanzo 1:2 Humpa msomaji hisia uwepo wa Mungu "hapo mwazo?"

_______________________________________________ Roho wa Mungu alikuwepo

Roho wa Mungu alukuwa “akielea juu ya” maji . Kuna hisia kuwa jambo fulani linakwenda kutokea. Picha ni kama ya uwepo wa mzazi yeye humfunika mtoto. Kuna picha gani nyingine au maneno gani unaweza kutumia kuelezea ufunikaji wa Roho wa Mungu? Kumbu kumbu la Torati na Isaya vinaweza kusaidia. Angalia!

• Kumbukumbu 32:11 - ____________________________________________________

• Isaya 31:5 - ____________________________________________________________

**SALA:**

Bwana, Asante kwa uwepo wa uungu wako hata kabla ya uumbaji kuanza. Unaendelea kufunika juu ya vyote ulivyotengeneza. Asante kwa kutunza uumbaji wako, kazi ya mikono Yako. Asante kwa kunitunza na wote ninao wapenda.

_______________________________________________________________
_______________

_______________________________________________________________
_______________

_______________________________________________________________
_______________

## SOMO LA KWANZA ~~ SEHEMU YA 22

***Soma Mwanzo1.***

**ZOEZI:**

Kwenye sura hii tumegundua kuwa kama mwumbaji, Mungu alinena na uumbaji ukatokea. Mstari wa 3 ni mfano mmoja. Katika Zaburi 148:5 tunasoma "…Aliamuru na vikaumbwa." Sasa, orodhesha vitu vyote ambavyo Mungu aliumba kwa amri Yake. Jaribu kutafakari kufuatana na maelekezo mbalimbali na Baraka Alizotoa kwa vile alivyo viumba. Kwa mfano, katika mstari wa 3 "Alitenganisha" nuru na giza. Katika mstari wa 9 "Anakusanya" maji katika sehemu moja. Katika mstari wa 20, Anabariki viumbe na kuviambia "kuzaa na kuongezeka"
Siku 1: Mwanzo 1:3-5

______________________________________________________________

______________________________________________________________

Siku 2: Mwanzo1:6-8

______________________________________________________________

______________________________________________________________

Siku 3: Mwanzo 1:9-13

______________________________________________________________

______________________________________________________________

Siku 4: Mwanzo 1:14-19

______________________________________________________________

______________________________________________________________S 5: Siku 5: Mwanzo 1:20-23

______________________________________________________________

__________________________________________________________________________

Siku 6: Mwanzo 1:24-27

__________________________________________________________________________

__________________________________________________________________________

**ZOEZI:**

Kuna maneno yana jirudia katika sura ya 1. Tafuta maneno hayo na andika ni mara ngapi kiloa neno ni mara ngapi limetumika. Kumbuka: Huu ni muda wako mzuri wa kutumia kalamu yako ya kuweka alama. Weka alama kila mara maneno haya yanapotumika. Unaweza kutumia rangi tatu tofauti.

1. "Na Mungu akasema…" ,mara________
2. "Na ikawa hivyo." mara ________
3. "Na Mungu akaona kuwa ni vyema." mara ________

**SWALI: Tunajifunza nini kuhusu Mungu kutokana na mistari hii ya mfano?**

1. ________________________________________________________________________
2. ________________________________________________________________________
3. ________________________________________________________________________

Mungu ni muumbaji.Alinena, uumbaji ukatokea. Kila kitu alicho kiumba kilikuwa chema, chema sana (Mwanzo. 1:31).

**MASWALI YA KUTAFAKARI:**

Ninapo kumbuka kuwa Mungu ni muumbaji, ni lini na wapi ninapo Muona akifanya kazi ya kuumba  na kutunza vile alivyoviumba? Je kuna wakati ninaona kuwa "Amedondosha mpira" na ametelekeza vile alivyoviumba?  Nina jifuna nini kuhusu Yeye kama mtunzaji?

• Wakolosai 1:16, 17

________________________________________________________________

• Mathayo 6:25-34

________________________________________________________________

**KUCHIMBA KWA KINA:**

Mungu alikuwapo kabla ya uumbaji.Hakuumbwa.Ni wa milele. Daima Alikuwapo na Atakuwapo Katika Ufunuo1:8 Anatajwa kama__________________________ na __________________________. Katika Ufunuo 21:6 tena Mungu anatajwa kama ____________________________ na __________________________. Kwasababu tumetekwa na muda, kila jambo kwetu lina mwanzo. Fikiria vile vitu ambavyo vimekuwa mwanzo kwako. Labda unakumbuka kuzaliwa kwa mtoto, au siku ya kwanza ya shule, au wakati muhimu wa wazo la kujenga. Kwenye daftari yako andika orodha ya myanzo ambayo inakuja kwenye mawazo. Mungu alikuwapo kabla ya mwanzo. Siku zote alikuwapo.

**SWALI LA KUTAFAKARI:**

Ni swali gani linalokupa changamoto pale unapokumbuka kuwa Mungu ni wa milele, Alfa na Omega, Mwanzo na Mwisho?

**SALA:**

Bwana, leo ninakushukuru kuwa Wewe ni Muumbaji wa viumbe vyote. Hapo mwanzo uliamua kuumba mbingu na dunia. Kila kitu ulicho kiumba kulikuwa chema na kizuri sana. Asante!

## SOMO LA NNE ~~ SEHEMU YA 33

Mwazo2:1Inasema kuwa uumbaji ulikamilika. Na tena, tunasoma 2 na 3. Andika mistari hii:

________________________________________________________________
________________
________________________________________________________________
________________
________________________________________________________________
________________

**SWALI:**

Kwa maneno yako, ni mambo ganiyatokea katika siku ya 7 (mwanzo 2:2, 3)?

________________________________________________________________
________________
________________________________________________________________
________________

**FUNDISHO:**

Jinsi Mungu alivyo chagua kuibariki siku, siku ya saba, aliifanya takatifu ilikuwa ni siku yake ya kupumzika. Aliitakasa , Aliamua kuitenga kwa makusudi fulani; Makusudi yalikuwa ni kupumzika.

- *MAFAFANUZI*: ***Takasa*** ina maana kuifanya maalumu.
- *MAFAFANUZI:**Siku ya Sabato,***siku ya kuabudu na kupumzika.Kumbuka: Kwa Wayahudi Jumamosi ya kawaida imetengwa kama siku ya Sabato; pamoja na hayo, waamini wa kwanza walichagua Jumapili kusherekea kufufuka kwa Yesu. Umuhimu siyo ni siku gani katika juma, bali kwa mfuatano wa kila siku ya saba ni siku ya Sabato.

Mungu alitoa maagizo kwa maisha ya uumbaji yaliyoumbwa. Alichagua kufanya kazi siku sita na kwa siku ya saba alipumzika. Mungu alihitaji siku ya kupumzika? Mungu alikuwa amechoka? Kama Mungu wa mahusiano, aliamua kupumzika ili afurahie maisha pamoja na uumbaji wake.

Mwingine huwaza kuwa Alitaka tu kusherekea. Mwanzo 1:31 inasema kwamba Aliona vyote, na akaona kuwa ni vyema. Mwingine anashangaa kama kweli aliona miti au wanyama au Adamu na Eva na akasema maneno kama "Nilifanya kazi nzuri kama hii nilipo kuumba!" Kwa siku sita watu wana nafasi ya kufanya kazi, lakini siku ya saba wamepewa nafasi ya kupumzika kazi zao. Ni siku ya kujali mahusiano ---kwanza, uhusiano na Mungu na tena uhusino tulio nao na nafsi zetu, pamoja na wengine, tukijumuisha familia na marafiki. Ni siku ya kufurahia uumbaji. Kwahiyo hii ni siku katika juma, iliyotengwa kwaajili ya *kuabudu* huku tukitafakari mahusiano na Mungu.

Mungu alijua kuwa tunahitaji muda wa kumuabudu, ili kutunza nafasi nzuri ya mahusiano kati ya Muumbaji na vilivyo umbwa. Aidha alijua kuwa tunahitaji siku ya *kupumzika* kwa ajiri ya miili yetu na fikra, ili tuweze kufanya vizuri kwa siku nyingine sita. Na Mungu alijua kuwa tunahitaji muda wa kupumzika na familia, na marafiki, ambao ni sehemu ya jamii ya maisha yetu, na mwisho, alitaka tufurahie mahusiano aliyotupatia, pamoja na maumbile na vyote alivyo vifanya.

**ZOEZI:**

Neno la Mungu linazunguzia juu ya siku ya Sabato. Hebu tuchukue muda wa kujifunza kile Anacho sema katka kurasa zifuatazo.

• Kutoka 16:23

______________________________________________________________

______

• Kumbukumbu 5:12-15

______________________________________________________________

______

• Isaiya 58:13-14

______________________________________________________________
______

**MATUMIZI YA ZOEZI:**

Ukiwa na mawazo ya hitaji letu la kupumzika na kuabudu, andika kwenye daftari yako, ni ipi iliyo Sabato ya kweli, siku ya mapumziko, inavyo weza kufanana katika maisha yako. Onyesha badiliko moja au mawili ambayo ungetaka kufanya ili kutakasa siku ya sabato, huku ukikumbuka mahusiano.

1. Nikikumbuka mahushiano yangu na Muumbaji wangu, ningetaka kufanya mabadiliko yafuatayo:

______________________________________________________________
_______

2. Ninakumbuka uhusiano wangu na mwili wangu na mawazo yangu, ningetaka kufanya mabadiliko yafuatayo:

______________________________________________________________
_______

**3.** Wakati nikikumbuka uhusiano wangu wa kijamii na jamaa zangu, hasa familia yangu na marafiki, pamoja a maumbile ningetaka kufanya mabadiliko yafuatayo:

______________________________________________________________
________

**SALA:**

Mungu, Wewe ni Muubaji wangu.Nakushukuru kwa zawadi ya kupumzika. Mara zote najikuta nikifanya kazi masaa 24 kwa siku 7.

Neno lako lina nikumbusha kuwa nina hitaji Siku ya Sabato ninapo weza kukuabudu na kuimarisha mahusiano niliyo nayo pamoja na wengine, niki jumuisha na nafsi yangu. Naomba nipate pumziko langu ndani yako.

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

## SOMO LA KWANZA ~~SEHEMU YA 44

**ZOEZI:**

Katika Mwanzo1:26 Mungu alisema, "Hebu na tuumbe mtu kwa mfano Wetu…" Biblia inaendelea zaidi iki elezea habari ya uumbaji wa Adamu na Eva. Sura za 1 na 2 hutoa maelezo tofauti kwa sababu hizi habari mbili ziliandikwa kwa malengo na makusudi tofauti
Hebu tuanze kwa kutafakari habari kufuatana na uumbaji wa mwanadamu kutoka kila sura. Unapata ujumbe gani kuhusiana na uumbaji wa mwanadamu kutoka kwa kila mstari? Usi husike zaidi na idadi ya nafasi wazi zilotolewa, ila jaribu kuonyesha ni upi ulio ukweli ulio funuliwa kufuatana na uumbaji wa mwanamume na mwanamke.

**Kutoka Mwanzo 1:**

"Mwanadamu" lina maana ya wote wawili____________________________. ("wao"—mstari 27).

• Mstari 26:

Mwanadamu ametengenezwa kwa mfano wa Mungu,kwa mfano wake wanapaswa kutawala uumbaji.

• Mstari 27:

__________________________________________________________________________________________________

• Mstari 28: __________________________________________________________________________________________________

• Mastari 29: __________________________________________________________________________________________________

**Kutoka Mwanzo 2:**

Jina la mwanadamu ni nani? ___________________ (Mwanzo 2:20) Jina la mwanamke ni nani? ____________________________ (Mwanzo 3:20)

• Mstari 5: __________________________________________________________________________________________________

• Mstari 7: __________________________________________________________________________________________________

• Mstari 18: __________________________________________________________________________________________________

• Mstari 20: __________________________________________________________________________________________________

• Mstari 21: __________________________________________________________________________________________________

• Mstari 22: __________________________________________________________________________________________________

• Mstari 23:

______________________________________________________________________
_________

**FUDISHO:**

Mwanzo1:27unataja mtu huyo, wote mwanamume na mwanamke, wame umbwa kwa mfano wa Mungu. Hii imebeba picha yenye nguvu kwaajiri yetu kama uumbaji wa Mungu. Mungu anatupatia wajibu wa kuonyesha taswira ya uumbaji. Kioo
Kioo huonyesha taswira ya sura . Taswira ni sura halisi. Mpango wa Mungu ulikuwa mwanadamu awe taswira yake ulimwenguni. Mwanadamu hubeba sura na huonyesha, tunaumba (tengeneza) vitu, tunapo shirikiana, tunapo chagua, tunapo penda, tunapo abudu, na kuishi katika uhusiano pamoja naye. Mungu aliwapa wanadamu makusudi ya masisha yao kwa kuwaida, kwa kuwapa wajibu wa kuonyesha sura yake.
**SWALI**: Mungu alikuwa amewapa Baraka gani katika Mwazo:28?
1. Kuwa________________________________ na
_______________________________
2. ___________________________ dunia na
_____________________________ ina.
3. ________________________________samaki, ndege, na kila kiumbe kilicho hai.

**MASWALI YA KUTAFAKARI:**

1. Uliisha fikiri kuwa maisha yako hayana maana wala makusudi yoyote?
2. Kadiri unavyotafakari juu ya mistari hii unaamini thamani Mungu aliyo weka kwenye maisha yako ni ipi?
______________________________________________________________________
_________

Ni nyakati gani unapo kuwa na ushirikiano na Mungu ukiwa kama aliyeumbwa?

______________________________________________________________________

3. Inaleta tofauti gani katika maisha yako ukifahamu kuwa Mungu amekubariki na amekuita ili kumdhihirisha ulimwenguni unamoishi?

______________________________________________________________________

**KUCHIMBA KWA KINA:**

Chukua nafasi kusoma Zaburi ya 139. Tafakari zaidi mistari ya 13-16, ukifahamu jinsi Mungu anavyo jali kazi ya uumbaji wake ambao umebarikiwa naye na unaitwa kumdhihirisha. Ni maana gani ya kina ambayo mistari hii inatoa kuhusiana na mahusiano Mungu aliyo nayo na uumbaji wake hata kabla ya kuzaliwa.

______________________________________________________________________

Uumbaji hutufundisha juu ya mahusiano yatu nay eye. Zaburi ya 8:3,4 inatuambia nini kuhusiana thamani yetu kwake?

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

Ni fundisho gani 1 Chronicles 29:14 inalotoa tunapokumbuka vile tunavyo dai kuwa vyetu?

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

**SALA:**

Ee! Mungu, Si kwamba ume niumba tu, bali ume bariki na maisha yangu kwa makusudi na malengo. Ume niitaka katika ushirikiano na Wewe na umenipa jukumu la kukudhihirisha kwa vyote vilivyo umbwa. Nina kushukuru kwa kuwa nguvu yako inafanya kazi ndani yangu.

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

## SOMO LA KWANZA ~~ SEHEMU YA 55

**FUNDISHO:**

Kwa mfururizo, Mwanzo 2:24 itakuwa ikisomwa wakati wa harusi au utakuwa ni ujumbe wa msingi kwa mtumishi wa Mungu kwa ajiri ya bwana na bibi harusi. Mwanzoni kabisa Mungu aliamua kuanzisha ndoa, muunnganiko wa mwanamume na mwanamke. Ndoa ilikuwa ni sababu

kwa mwanamume kuacha baba yake na mama yake na kuungana na kuwa mwili mmoja na mke wake. Ina furahisha kusikia kwenye kifungu hiki kuwa ndoa ni wawili kuwa mwili mmoja. Neno "nina" halisababishi badiliko la ghafla la watu wawili tofauti kuwa mmoja. Ni *mchakato* wa kuwa mmoja na mchakato huo utaendelea maisha yote ya kuishi pamoja. Mchakato wa kuwa mwili mmoja unaanzishwa na tendo la ndoa. Mstari wa 25 unazunguzia habari za mke na mme kuwa uchi na kutoona aibu. Kushirikiana kwa uchi kati ya mwanamume na mwanamke ilikuwa ni uzuri wa Mungu, na makusudi ya neema yake alipoumba mwanamke na kumkabidhi kwa mwanamume kama mke wake.

**SWALI:**

Rejea ya Biblia iliyo zoeleka ambayo ina ongelewa mara nyingi kwenye harusi ina chukuliwa kutoka Mathayo 19:6.Onyesha kifungu. Kusudi la Mungu lilikuwa nini kufuatana na mstari huu?

______________________________________________________________

____________

**KUCHIMBA KWA KINA:**

Vifungu vingi kwenye Biblia vinafanya rejea juu ya ndoa na makusudi ya Mungu kwa mwanamume na mwanamke kuungana katika ndoa. Ikiwa una taka mafunzo zaidi juu ya somo hili baadhi ya mistari inaweza kuwa msaada kwako katika kuanza mafunzo hayo. Matumizi ya mistari rejea iliyo onyeshwa katika mistari ya pekee itakuongoza katika vifungu vya ziada kwa kukumbuka.

- Waefeso 5:21-33
- 1Wakorintho 13 (Hii ina fahamika kama sura upendo)
- 1Petro 3:1-7

**MARUDIO:**

Katika masomo ya juma hili tume muona Mungu kama Muumbaji wa mbingu na nchi na tume mtambua kama wa milele, hakuumbwa na alikuwapo kabla ya kuanza kwa nyakati.
Tuliona siku za uumbaji ambazo zina hitimishwa na siku takatifu,siku iliyo takaswa, siku iliyo tengwa kwa ajiri ya kupumzika. Tuliona kwa ufupi uumbaji wa mwanadamu na maelezo ya Mungu kuhusu makusudi ya kuwaumba kwao. Tume liona kwa ufupi uumbaji wa mwanadamu na maelezo ya makusudi ya Mungu amabayo ni kumdhihirisha duniani. Na tume ona ndoa na makusudi ya Mungu kwamba mwanamume na mwanamke wawe mwili mmoja. Mungu aliumba na kutamka kuwa vitu vyote ni vyema. Kila kitu kilikuwa mahali. Vyote vilitengeneza na Yeye kumpa utukufu na heshima. Kuna jambo lingine moja……

**SWALI:**

Mwanzo 2:8-9 inasema kuwa Mungu alipanda bustani iliyoitwa ____________________________.
Miti miwili ilipandwa katikati ya bustani. Iliitwa: 1. ___________________________________________________________

2. ___________________________________________________________

Mstari wa15 Mungu alimpa maelekezo mwanadamu kuhusu bustani ya edeni. Alipewa maelekezo gani?

_______________________________________________________________

_______________________________________________________________

Ni ipi amri moja ya Mungu kwao? Andika mistari ya 16 na 17:

_______________________________________________________________________

_______________________________________________________________________

_______________________________________________________________________

_______________________________________________________________________

Mungu alisema kuwa matokeo ya kuto tii yange kuwa nini?

_______________________________________________________________________

Mwanzoni unaweza kupona kuwa Mungu hakutenda haki kwa kuweka "mti wa kujua  meme na mabaya" bustanini na kuonekana kama jaribu kwa Adamu na Eva. Lakini tukumbuke kuwa Mungu alimuumbia mwanadamu na uwezo wa ihari wa kuchagua kutii au kuto tii Neno lake. Miti hii ilikuwa katkati ya bustani.Walikuwa wakizungukwa na uzima. Mungu anataka maisha yetu yazungukwe na Neno lake.

**SWALI LA KUTAFAKARI:**

Ina maana gani kwako kuishi na Neno la Mungu likiwa katikati ya maisha yako?

_______________________________________________________________________

_______________________________________________________________________

_______________________________________________________________________

Kwa nyongeza ni kwamba Mungu hakudai kwamba wampende. Upendo ni chaguo, na mti ulikuwa ni chaguo moja, ambalo wange fanya ambalo linge onyesha upendo wao kwake. Hipendezi kuona kuwa vitu vyote Mungu alivyo umba, katika vitu vyote ambavyo Mungu aliwapa

kuvifaidi, pamoja na vyote Mungu alivyo weka bustanini kwa chakula chao, pamoja na vyote walivyo pewa kutokana na ukarimu wa Mungu, mti huu tu ulizuiwa. Simulizi hii inaendelea wakati Somo la 2 linadaanza majadiliono kuhusiana na mti…….

## SOMO LA PILI ~~ SEHEMU YA 11

**UTANGULIZI:**

Mungu akatazama vyote alivyo viumba akatoa tamko kuwa ni vyema, vizuri sana. Katika siku ya sita Mungu alimuumba mwanamume na mwanamke. Vyote alivyo vitengeneza alivitayarisha kwa ajiri yao, alivikabidhi kwao, na vinge tumika kukidhi mahitaji yao. Matunda ya miti yote yalikuwa “yaki pendeza macho na yalifaa kwa chakula” (Mwazo 2:9) na akawambia kuwa yalikuwa kwa ajiri ya chakula chao (Mwanzo 2:16). Pia Mungu alipanda katikati ya bustani mti wa kujua mema na mabaya. Kwa maelekezo waliyo pewa mwanamume na mwanamke ni kwamba, hawakupaswa kula chochote toka mti huu (Mwanzo 2:17). Mungu aliwaambia kuwa kama wange kosa utii wakala kutoka mti huu wangekufa. Kwa vyovyote, hii ilionekana kueleweka. Miti yote bustanini ilikuwa yao, ya kula na kufurahia. Mti huu mmoja tu;  ulizuiwa. Huu ni wema wa kutosha. Mungu alitoa kwa kiasi kikubwa kwa ukarimu kwa ajiri ya maisha bora bustanini.

Soma Mwanzo 3.
**SWALI**: Ni tabia gani inaelezwe katika mstari wa 1?

______________________________________________________________

____________

**Zoezi:**

Kupata uelewa mpana juu ya nyoka angalia rejea zifuatazo, na andika maneno yaliyo tumika kuelezea kiumbe huyu:

**Rejea za maelezo**
Mwanzo 3:1
Luka 4:2
Yohana 8:44
2 Wakorintho 11:3
Waefeso 6:11
1 Petro 5:8
Ufunuo 12:9

Angalia mlinganisho katika Yohana10:10. Shetani ame elezewa kama ________________________
Ambaye amekuja ________________________, _________________________________,na _______________________________________________.Yesu alikuja, kwa upande mwingine, kwamba
__________________________________________________________________
________________
__________________________________________________________________
________________
__________________________________________________________________
________________

**KUKARIRI:**

Maneno ya mwisho ya Yohana 10:10, ni mazuri kwa kukariri. Yaandike kwenye kijitabu chako, na chukua dakika chache kutafakari katika tofauti ambayo yage sababisha katika maisha yako, kwa kujua kuwa Yesu alikuja kukupatia uzima ambao ni kamili na wenye maana, uzima wa milele. Nakili maneno kwenye kijitabu chako. Na mwombe afungue moyo wako kuelewa maana ya kuwa na uzima wa milele pamoja naye kwako.

## SOMO LA PILI ~~ SEHEMU YA 22

**FUNDISHO:**

Majaribu hushambulia, na kuwa changamoto kwenye kiini na lengo la Mungu la kutuumba. Vishawishi hivi na majaribu yenye kudanganya hutokea kama kitu cha kuvutia, au kama jambo la ziada la kutii na kutumia kwa ajili ya maamuzi tunayofanya katika maisha yetu. Yana shawishi kwa sababu ni yenye kudanganya. Hii hutoa hali ya ziada ambayo huchanganya ukweli wa Neno la Mungu. Majaribu yametuzunguka pande zote katika ulimwengu tunamoishi. Kujaribiwa si shida, ila kushindwa na majaribu ndio udhaifu. Tatizo ni kugundua uwezo wa majaribu wa kutufanya tushindwe kugundua tofauti ya mema na mabaya. Majaribu ni uongo. Pale tunapoyakubali na kumeza anasa zake za uogo, matokeo yake ni kuteswa na kushitakiwa na dhamira zetu na kuaibika. Hii yote hutuondolea furaha ya maisha kamili na uhuru ule ambao Yesu ana uzunguzia katika Yohana 10:10. Habari inaanza. Soma Mwazo 3:1-7.

**MASWALI:**

Nyoka na mwanamke wana kutana. Nyoka analeta changamoto. Nyoka alimwambia neno gani mwanamke?

______________________________________________________________________
________________

______________________________________________________________________
________________

Ni maneno gani ya Mungu yaliyokuwa ya kweli katika Mwanzo 2:16?

______________________________________________________________________
________________

________________________________________________________________________________

Itikio lake ni nini 2?

________________________________________________________________________________

________________________________________________________________________________

Ni neno gani la Mungu la kweli katika Mwanzo 2:16, 17?

________________________________________________________________________________

________________________________________________________________________________

Katika mstari wa 4, tunaambiwa mbinu ya mjaribu aliyosisitiza. Ni itikio gani la nyoka kwa yale Mungu alyowaambia mwanamume na mwanamke?

________________________________________________________________________________

Uongo ni upi katika mstari wa 4? (tazama Mwanzo 2:17)

________________________________________________________________________________

Nyoka aliharibu ukweli wa maneno ya Mungu, kwa kutumia maneno ya uongo. Ni maneno gani ya nyoka katika mstari wa 5 hilo lilikuwa jaribu la mwisho?

"…macho yako yako yatafumbuliwa,

na______________________________________________________________________________

Swali la mwisho:

- Ni upi utakuwa mwongozo wako katika mazingira utakamo ishi?

Utawaamini akin a nani?

Changamoto ya mwisho:

- Ni nani ambaye maisha yako yatajengwa kwake?

**KUCHIMBA KWA KINA:**

Maswali katika mistari hii mitano ya Mwanzo3, ni changamoto kwa ukweli wa Neno la Mungu. Huwezi kusikia hata kidogo sauti ya ujanja ya majaribu katika kichwa chako ikinong'ona swali, "kweli Mungu alisema….?. Na swali la pili linakuwa la kijasiri na lenye changamoto zaidi: "Hivi kweli Mungu *alimaanisha* kile alichosema?"Neno la Mungu ni kweli? Ukweli unaweza kuwa chochote na mtu ndiye anayechagua kama ni kweli au ni uongo. Ni kweli kuwa Mungu huzungumza nasi kupitia Neno lake?Na kama anafanya hivyo, Je humaanisha kile anacho sema? Hebu tuone kile Mungu anacho sema katika Isaya 45:18-19.

• Humsema nani kuwa ndiye?

______________________________________________________________________

_________

• Wana sema nini kuhusu Neno analo sema ? Kumbuka mwisho wa mstari wa 19.

______________________________________________________________________

_________

______________________________________________________________________

_________

**MATUMIZI:**

Unaweza kujikuta ukiuliza baadhi ya mambo kwa mfano, unaweza kuuliza: Je kuna Mungu mmoja? Hivi aliye umba mbingu na dunia ni Mungu kweli? Hakuna Mungju mwingine? Kama Anasema ukweli kama asemavyo, Anafanya hivyo katika kifungu hiki cha Isaiah 45, Hiki kinasema nini juu ya nadharia tofauti zinazotolewa katka mila zetu za sasa ambazo hukiri imani zinazo pingana? Nitamwamini nani kuwa anasema kweli ikiwa kiloa mtu ana mawazo yake mwenyewe kuhusu

ulio ukweli? Pamoja na maswali tofauti yawezayo kuja katika mawazo, tutajua nini juu ya ukweli? Wakati mwingine mambo anayo sema Mungu, ni mema sana kiasi cha kuyatilia mashaka kama ni kweli.

• Kwa mfano katika Yeremia 31:3 Anasema“Nimependa

________________________________________________________________
_________
________________________________________________________________
_________

Hapo ninakumbuka nyakati zile ambazo nilichukizana na rafiki niliyempenda wakati Mungu ana niambia kuwa ana nipenda kwa upendo usio na mwisho.

• Tena katika Warumi, 8:38-39 Ana niambia kwamba“…wala

________________________________________________________________
_________
________________________________________________________________
_________
________________________________________________________________
_________

Hakuna kitu kinacho weza kunitenga na upendo wa Mungu. Je inaweza kuwa ukweli kuwa hakuna kinacho weza kunitenga na upendo wa Mungu wakati nikikumbuka yale yote yaliyo nitenga na wengine katika maisha yangu? Swali lililo tungwa na nyoka katika bustani lime endelea miaka yote na yana ulizwa na mini leo. Kufuatana na Yeremia 31 andika maswali mawili:

• Ni kweli kuwa Mungu alisema

________________________________________________________________

• Ni kweli alimaanisha

________________________________________________________________

Kufuatana na Warumi 8 andika maswali mawili:

• Ni kweli Mungu alisema

________________________________________________________________

• Ali maanisha

________________________________________________________________

**SALA:**

Bwana,Nina jitahidi kujua ukweli. Nataka kujifunza zaidi juu ya yale ambayo unge niambia. Nisaidie kufahamu, kuelewa na kukubali kuwa Neno lako ni ukweli. Fungua moyo wangu kuamini kuwa “unasema ukweli” na “kutamka yaliyo haki”

__________________________________________________________________

_________________

__________________________________________________________________

_________________

__________________________________________________________________

_________________

## SOMO LA PILI ~~SEHEMU YA 33

**FUNDISHO:**

Tikirudi nyuma katika Mwazo 3, swali linaendelea kubaki: Kwa nini Mungu aliumba mti na kuamru mti ule ule, mti wa ufahamu wa mema na mabaya, na kuweka amri ya kuto ula? Zaidi ya hayo, kifo ilikuwa ni hukumu kwa kuto tii amri hiyo. Tuki rudi kwenye mtazamo wa kwanza, ina onekana kama ni madai yasiyo ya haki na adhabu katili. Kwa sababu Mungu husema kuwa ni Mungu wa upendo na akatoa adhabu kali haieleweki.

Hebu tufikirie baadhi ya mambo. Kwanza, tuna hitaji kufahamu kuwa Mungu ni Mungu wa mahusiano. Ni yeye aliye umba na ndiye anaye endelea kuhusika kwa upendo vile vyote alivyo viumba. Kwa namna fulani, ni uhusiano wa kama uhusiano wa mtoto na mzazi. Mungu aliamua mzazi ahusike katika kuumba mtoto. Na ali kusudia kuwa mzazi aendelee kuhusika katika maisha ya mtoto na kumtunza. Mungu kwa ukamilifu huanzisha uumbaji wake na kuutunza; haachi vile alivyo viumba. (Isaya 49:15).
Kwa wakati huo huo, ni muhimu kuelewa ukweli wa upendo wa Mungu ulio kusudiwa. Upendo ni uchaguzi, ni tendo la hiari. Si hisia. Mtu hufanya uchaguzi wa kupenda. Hakuna mtu anaye weza kukufanya umpende mtu au usimpende. Utii ni maelezo ya chaguo la kupenda. Mzazi humpenda mtoto na mtoto huitikia upendo kutokana na chaguo la kupenda lilofanywa na mzazi. Mipaka ambayo mzazi huimarisha nyumbani huipa familia mazingira ambamo huonyeha upendo wao kwa wao. Mtoto, wanandoa, na hata wazazi wanapewa fursa ya kupenda kwa kuheshimu na kutii hiyo mipaka.

Ina tupasa pia kukumbuka kuwa Mungu ni Muumbaji na kwamba mwanamume na mwanamke walikuwa ni walio umbwa. Mwanamume na mwanamke iliwapasa kuelewa na kuishi kwenye mahusiano. Mti ulizuiwa si kwamba Mungu aweze kuwaangalia ili wakikosa utii kama alivyojua kuwa wangefanya, badala yake mti ulizuiwa ili kuwapa wote wawili mwanamume na mwanamke fursa ya kumfahamu Mungu kuwa kama alivyo, akiitwa Mungu. Ilikuwa ni fursa yao kufahamu uumbaji wake wa thamani na kuonyesha upendo kwake, kumtii ikiwa ni tendo la upendo; kwahiyo, kujitoa kutii mamlaka yake juu yao.
Katika Mwanzo3:5, Swali la mwisho la nyoka ni swali la nani atakuwa Mungu. Hadi mtoto anapokuwa mtu mzima, swali hubaki: Nani atakuwa mzazi? Mungu alitaka viumbe vyake kupata usalama katika kufahamu uhusiano wao na Yeye. Alikuwa ni Mungu, Muumbaji wao, na wao walikuwa viumbe wake.

Alitaka tu wafahamu wema wake. Aliueneza kupitia vyote alivyo vitengeneza. Alitaka wafurahie uhusiano wa upendo pamoja naye na wao kwa wao. Alitaka wabebe mzigo wa wajibu wa kufahamu mabaya na alitaka kuwalinda kutoka kwenye utawala na nguvu za mabaya. Upendo wake kwa vyote alivyoviumba, hasa kwa uhusiano wa upendo na wanadamu, ulikuwa ni bora ila alipenda kuwapa fursa ya kuonyesha upendo wao kwake kupitia utii wao kwake.

Tukiwa na jambohili kwenye mawazo yetu tufungue Mwanzo 3:6. Andika hii mistari ukikumbuka faida ya kila neno.

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

"Alichukua baadhi akala. Na mengine akampa mme wake…na akala."

**KUTAFAKARI:**

Tumia muda mfupi wa kutafakari. Andika baadhi ya mawazi yako kwenye daftari yako, kuhusu kile ambacho kimetokea sasa hivi. Ni kipi ambacho kingekuwa kama ni kufahamu wema wa Mungu na ukarimu wake na sasa umedanganywa katika kulikuwa na zaidi?
Mwanzo 3:7 unasema, "macho yao wote wawili yalifumbuka…" Ni lipi la kuogopesha katika kutii na kufuata uongo? Kumbuka fikra nyingine zinazokuja kwenye mawazo yako

**MATUMIZI:**

Kutafakari kwako kunaweza kukuelekeza katika wakati wa nafsi yako kushawishika.

1. Kumbuka wakati uliposhindwa na majaribu, ulipoasi, ulipokosa kutii, ilikuwa ni hali gani?

2. Kumbuka wakati ulipoona upendo na msamaha wa Mungu kupitia maneno na matendo ya mtu mwingine. Alikuwa ni nani, na maneno na matendo yake yalikuwa ni yapi, ambayo yalikuletea upendo na msamaha wa Mungu?

3. Tafakari ulipo pata muda wa kutoa upendo na msamaha wa Mungu kwa mtu mwingine, kwa sababu umeone nguvu ya upendo, msamaha wake wewe mwenyewe maishani mwako. Ni nani mtu huyo na ni kwa namna gani Mungu alikutumia kuleta upendo wake kwa mtu huyo?

**SALA:**

Mungu muumbaji, Ninaweza kukiri mbele yako kuto tii kwangu. Nime kuasi kwa njia mbalimbali kutokana na mambo niliyo chagua kufanya, kusema, na kufikiri. Nina kuomba unisamehe na kuliweka maanani kuwa uliniumba kwa upendo na unataka niwe na maisha yaliyo kamili na kusamehewa kupitia Yesu, Mwokozi wangu.

______________________________________________________________________________

______________________________________________________________________________

______________________________________________________________________________

## SOMO LA PILI ~~ SEHEMU YA 44

**FUNDISHO:**

Hebu turudi tena kwa yale yaliyo tokea katika Mwanzo Genesis 3:6. Adamu na Eva walishindwa na macho yao yalifunguliwa. Ni rahisi sana kuwanyoshea kidole na kusema, "Kijana, ulikosea. Sisi tuliobaki hatuna fursa." Ni rahisi kufikiri kuwa sisi tuko salama kwa sababu tunao wa kulaumu. Hebu tutazame kwa karibu kiasi.

Mahali pa kuanzia ni kutafakari juu ya hamu amboyo imewekwa wazi. Labda tunda ambalo lina onekana katika Mwanzo 3 ni tunda la kawaida kama "tunda" linalo patikana kwenye maisha na mazingira yetu. Ni maneno gani yanayo tumika katika Mwanzo 3:6 kuelezea tunda?

- tunda la mti lilikuwa

____________________________________________________________

- tunda la mti lilikuwa…

__________________________________________________________

- tunda la mti lilikuwa …pia

__________________________________________________________________

Tunda lilikuwa linafaa kwa chakula, linapendeza macho, na linafaa kea maarifa.

Hamu ya kwanza ni tama ya kuwa na zaidi. Tuna onekana kuwa hatuna ya kutosha. Tamaa yetu ya kutaka zaidi ni uchoyo. Tunapo kuwa na pesa kidogo tunataka zaidi. Tunapo kuwa na tunambuliwa kiasi, tunataka zaidi. Tukitambuliwa zaidi tunataka zaidi ya hapo. Tunapo kuwa na roho ya kuto furahi na kuto tosheka, maisha yetu yanashindwa kudhihirisha shukrani na kufurahia kazi ya mtu mwingine. Jaribu letu ni maisha yetu kujengwa kwenye kupata, kuapata na kupata zaidi.

**SWALI LA KUTAFAKARI:**

Fikiria uliposhuhudia, au ulihusika, na hamu ya kutaka zaidi.…

• Iikuwa ni hali gani?

__________________________________________________________________

• Kulikuwa na tama gani ambayo ilikuwa na hamu iliyokuwa ikitaka zaidi?

__________________________________________________________________

• Matokeo yake yalikuwa nini?

__________________________________________________________________

__________________________________________________________________

Hamu ya pili ni tamaa ya anasa. Ikiwa kitamaliza shida zangu, ninakitaka. Kama kinaleta hisia nzuri, kama ni kitamu, kinapendeza, basi nikitaka. Hamu ya anasa ni uchoyo. Anasa huwa in mahitaji yanayo ongezeka. Anasa inawe kuwa tabia na baadae inakuwa ni ulevi. Anasa

inaweza kuua uwezo wa kufikiri, maamuzi ya kiafya, na mawazo yanayo weza kwenda zaidi ya nafsi ya mtu na mazingira yake.

Mwisho anasa inaweza kuhatarisha mahusiano. Inaweza kutokea nini katika uhusiano wa mtu na Mungu iwapo maisha ya mtu yata tawaliwa na anasa?

**SWALI LA KUTAFAKARI:**

Kumbuka ulipo gundua anasa kama tatizo katika maisha yako …

• Hali ilikuwaje?

______________________________________________________________________

• Kulikuwa na hamu gani isiyoisha?

______________________________________________________________________

• Matokeo yalikuwa ni nini?

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

Tamaa ya tatu ilikuwa ni hitaji la kuwa na hekima. Ufahamu ni mamlaka. Tukiwa na ufahamu zaidi tunaweza kutawala matendo yetu kuhusiana na watu wengine; tunaweza kujifanya kuonekana wema. Mamlaka hutuwezesha kuwa na utawala. Ulimwengu ni wangu na nina jitahidi kuushinda. Mamlaka hutufanya kuamini kuwa hatuhitaji mtu yeyote, na kuishi maisha ya kiburi na kujitegemea wenyewe, siyo kumtegemea Mungu kama muumbaji. Tena kumbuka kinacho tokea ikiwa mtu atajifanya kutafuta madaraka kuwa kiini cha kuishi kwake.

**SWALI LA KUTAFAKARI:**

Kumbuka hali ya ambaye uchu wa madaraka husababisha hali ya matatizo…

• Kulikuwa na hali gani?

______________________________________________________________________

• Ni tamaa gani ya madaraka iliyo pitiliza iliyo hitaji kudhibitiwa?

______________________________________________________________________

• Matokeo yake yalikuwa nini?

______________________________________________________________________

Mwisho, katika Isaya 14:13-14, Mungu kupitia Nabii Isaya, anafunua moyo wa binadamu. Mwanadamu aliyeumbwa anasemaje? Orodhesha “Nita…” tano.

1. Nita ______________________________________________________________

2. Nita ______________________________________________________________

3. Nita ______________________________________________________________

4. Nita ______________________________________________________________

5. Nita ______________________________________________________________

Kujisifu ni mwisho. Hili ni jaribu na ndilo mwanamke alilochagua. Ikitokea tukapuuzia yaliyo wazi hebu tuendelee. Mwanamke alikuwa wa kwanza kula. Ina onekana kuwa mwanamme naye pia, alitekwa kwa kusikiliza maneno tofauti zaidi ya yale ya Mungu, ambayo nyoka aliwaletea. Mwanamke alichukua baadhi ya matunda akala,“alimpa na mume wake, naye akala.”

**KUKARIRI:**

Kwa ukimya wa muda, tunaweza kumuona Mungu anaye tupenda na kumpelekea hali zetu. Fungu a) Warumi 3:23-24. Maneno ya mwisho kabisa katika mstari wa 22 yanasomeka,
"Hakuna tofauti." Kwa kuanza na maneno haya andika maneno ya mistari ya 23 na 24:
"Hakuna tofauti
______________________________________________
______________________________________________
____________
______________________________________________
____________
______________________________________________
___________"

Unatiwa moyo kukariri mistari hii miwili. Iandike kwenye kijitabu chako, na anza kuyaongeza kwenye maktaba yako ya kumbukumbu. Maneno haya hutukumbusha kwamba jambo moja ambalo wanadamu wote hushirikiana; ni kwamba wote wametenda dhambi na kupoteza utukufu wa mfano wa Mungu, ambao alikusudia wakati wa uumbaji wake (Mwanzo 1:27). Lakini wakati huo huo, mistari hii hutukumbusha kuwa tuna hesabiwa haki bure kwa neema yake kwa njia ya ukombozi ambao ulitokana na Yesu.

**UFAFANUZI:**

1. ***Kuhesabiwa haki*** – Mungu hashikilii dhambi zangu ili kuniadhibu. Sihitaji tena kuadhibiwa kutokana na dhambi zangu. Tofauti na kuhesabiwa haki ni hukumu. Nime tangaziwa na Mungu kutokuwa na hatia. Ana niambia kuwa uhusiano umerudishwa. Maisha ya Yesu

ambayo hujumuisha kuteswa na kuuawa, vilifanyika kwa ajili yangu. Ame nifanya mwenye haki mbele zake.

2.***Neema***

Mungu hunipa upendo wake ambao siwezi kuupata mwenyewe wala kuustahili. Adhabu kwaajili ya dhambi ni ni kifo. Hii ndiyo stahili yangu. (Angalia Mwanzo 2:17 na Warumi 6:23.) Kwa adhabu na mauti ya Yesu nina pata upendo wa Mungu ambao sistahili, Neema yake na upendo huniweka huru kuishi naye milele.

3. ***Ukombozi***

Mungu alitaka kununua, au kukomboa, vyote vilivyo kuwa vime potea kutokana na dhambi. Utakatifu wangu ulipotea. Uhusiano wangu na Yeye ulipotea. Ni kama nilikuwa mtumwa wa dhambi, kwa mauti, na kwa shetani. Gharama ya kuninunua tena kutoka "utumwa" ilikuwa ni uhai wa mtoto wake, Yesu.

Ukombozi ni kitendo cha Mungu kuninunua na kuniokoa kutoka kwenye mateso, kutoka hukumu ya kifo iliyotolewa kwangu, kutokana na dhambi zangu. Alifanya hivi kwa kutumia maisha yake matakatifu, kifo, na kufufuka kwa Yesu, Mkombozi wangu.

Kumbuka: Maneno haya yatarudiwa kwenye mfururizo wote wa masomo haya. Kwasababu hiyo unatiwa moyo kujizoeza maneno haya yaliyo tumiwa kwenye kifungu hiko. Mafafanuzi haya uyaongeze kwenye yale uliyoandika katika kitabu chako, kwaajili ya rejea za baadae. Aidha uyaongeze kwenye kitabu chako cha maana za maneno.

**SALA:**

(Kumbuka tena Warumi 3:23-24).Bwana, Ninajua kuwa nimetenda dhambi na sina stahili nyingine ila mauti ya milele. Asante kwa ajili ya Yesu ambaye amenihesabia haki, Aliye ninunua na kuwa wako tena.

Asante kwa kutoshikilia dhambi zangu na kunihukumu kutokana nazo, kwa kunisamehe, kwa kunihesabia kutokuwa na hatia. Asante kwa neema yako, kwa upendo wako ambao sistahili. Asante kwa ajili ya Yesu, Mkombozi wangu, ambaye ame niweka huru kuishi na kunifanya niwe wako kwa kupitia msamaha wa dhambi.

_____________________________________________________________
_______________
_____________________________________________________________
_______________
_____________________________________________________________
_______________

**SOMO LA PILI ~~ SEHEMU YA 55**

Sehemu hii ya Somo la 2 lita husika hasa na Mwanzo 3:7-13. Katika Somo la 3 titakamilisha somo la Mwanzo 3 na tuta endelea na somo la habari ya Kaini na Abeli katika sura ya 4. Dhambi imeingia duniani. Mwanzo3:7 fafanua kulitokea nini baadae. "Tena…

- macho _____________________________________________________________
- na waka _____________________________________________________________;
- kwahiyo waka __________________________________________________________ na
- walifanya _____________________________________________________________
_."

Kutotii kuna matokeo. Sheria za barabarani zikivunjwa matokeo ni kulipa faini. Kama mtoto atavunja sheria ya wazazi, au za watu wengine walio kwenye mamlaka , mtoto ana adhibiwa. Matokeao ya kuto tii kwa mwanamume na mwanamke yalitokea mara moja, baada ya kuto tii

sheria ya Mungu ya kuto kula matunda ya “mti wa ufahamu wa mema na mabaya”. Walikabiliana na mambo ambayo Mungu hakukusudia yawapate.

Hebu tuangalie. Soma mistari 7-13 kwa wakati huu.

**MATOKEO #1:**

Tokeo la kwanza kabisa la dhambi ni *aibu*. “Walijijua kuwa wako ___________________”
Mwanzo 3:7). Walifahamu mema, sasa wame ahamu na mabaya. Kwa hiyo, ufahamu mkubwa unaanza.
Kitu cha kwanza walishona “______________________________ wote wakajifanyia
______________________.” Aibu yao ikawafanya watengane kwa hiyo wakajitengenezea vya kujisetiri. Ukaribu wao kukaisha sasa wana jiandaa kufanya kwa chochote kitakacho tokea kati na juu yao.

**MATOKEO #2:**

Soma mistari 8-10. Matokeo ya dhambi yanayo onekana yaliyo fuata yalikuwa ni *hatia.* Hatia hutufanya tutake kujificha. Mstari 8 unasema, “…na waka ___________ kutoka kwa __________________________ kati ya ________________ ya bustani.” Vile Mungu alivyo viumba wavifurahie sasa vinatumika kujifunika na kujificha uso wa Mungu, ambaye aliwaumba na kuwafurahia kama marafiki. Walikuwa hawana cha kumwogopa. Sasa wanajificha uso wake.
“Lakini Bwana Mungu alimwita mwanamume,
“_________________________________________________________
____________?”
Na mwanamume akasema,

_______________________________________________________________
_______________

_______________________________________________________________
_______________

Utakatifu ulikuwa umetoweka. Tangu kuumbwa walikuwa hawafahamu kuwa wako uchi. Hivyo ndivyo Mungu alikusudia waishi naye kama mme na mke. Nani aliye waambia? Aibu na hatia vilifunua dhambi yao. Kwa sababu ya dhambi walijitambua kuwa wako uchi, na kutokana na hatia yao waliogopa na wakajificha.

**SWALI:**

Labda hatuko tofauti kiasi hicho. Wajibu wetu kwa mwingine ni nini p-ale tunapo kamatwa? Siyo nani aliyekwambia?
Haina maana! Kwa haraka tunataka kwenda mafichoni. Hatupaswi kutumia vichaka kama sehemu ya maficho lakini mara nyingi tunajificha.

- Je unapata shida kutambua aibu na hatia yako juu ya maovu yako uliyotenda zamani?

_______________________________________________________________
_______

- Ni “vifuniko” gani ulivyotengeneza ili kujaribu kujificha wengine?

_______________________________________________________________
________

_______________________________________________________________
________

- Unakwenda wapi ili kujificha wakati ukiogopa kuonekana kwa yale uliyofanya?

_______________________________________________________________
________

_______________________________________________________________
_________

**MATOKEO #3:**

Matokeo ya tatu yanayo onekana ni hitaji la kuweka lawama kwa mwingine au kitu kingine. Katika mstari wa 11 Mungu anauliza.
“Ume _______________________________________________________________
_____
_______________________________________________________________
________________
_______________________________________________________________
_____________?”

Ni nini itikio la mwanamume?
“ _______________________________________________________________
__________
_____________________________________________________________ na akala .” Siyo
Adamu peke yake alijaribu kuweka lawama kwa mwanamke na kwa Mungu! “Mwanamke
Uliye nipatia…” Baadae Mungu akamwambia mwanamke na akauliza,
“_______________________________________________________________
_____________?”

Mwanamke naye anatafuta mahali pa kuweka lawama, kwahiyo anasema,
“_______________________________________________________________
________________
_______________________________________________________________
_____________.”

Lawama huwa inatafuta mahali pa kupumzika. Lakini, lawama inafanya nini kwa mahusiano? Lawama hutenganisha mwanamume si na mke wake tu kama tusomavyo katika mstari wa 7, bali lawama humtenganisha na Mungu, Yeye apendaye Alivyo viumba na alivitakia mema vyote alivyo vifanya.

**REFLECTION:**

• Chukua mda kutafakari juu ya vitu ambavyo Mungu analaumiwa.
• Kumbuka wakati wewe unapo husika kueneza lawama.
• Dhambi hutusababisha kukataa kuchukua wajibu kwa mawazo na matendo yetu. Mara zote mtu mwingine au kitu kingine, badala ya kuwa sisi kujilaumu
Ingeleta fofauti gani ikiwa wewe ungebeba wajibu na siyo kutafuta mtu mwingine wa kulaumu, ukijumuisha na Mungu ?

____________________________________________________________________________________

____________________________________________________________________________________

____________________________________________________________________________________

**SALA:**

Bwana Mungu, Mimi ni mwenye dhambi. Ninatuhumiwa kwa aibu, hatia, na kushindwa kwangu kuchukua wajibu, kwa maamuzi juu ya maisha yangu mwenyewe. Unisamehe kwa vitu nilivyo sema nilivyo fanya kwamba nilisababisha matengano kati yangu na wale ninao wapenda. Nisamehe kwa kufanya vitu ambavyo nimefanya vikanitenganisha na Wewe. Nina amini kuwa mimi ni mtoto wako kwasababu nimehesabiwa haki, nimepokea neema yako ya bure, na

nimekombolewa kwa damu ya Yesu. Kwa sababu hiyo ninakupa shukrani zangu na sifa.

_______________________________________________________________________________

_______________________________________________________________________________

_______________________________________________________________________________

## SOMO LA TATU ~~ SEHEMU YA 11

**UTANGULIZI:**

Hatujaribu kuachia hapo katika habari ya uubaji, tukiwa tumeshitakiwa na aibu yetu, hatia, na kushindwa kuchukua wajibu kwa mawazo yetu na matendo yetu. Kumbuka maneno katika Yeremia 31:3 – "Nimewapenda na upendo wa milele …" . Moja kati ya dhana isiyoeleweka kuhusu Mungu kwa hatua hii katika simulizi za Mwanzo 3, ni kwamba Mungu amechoka, kuweka laana juu ya uumbaji.

Dhana inayokuja ni kwamba Mungu ana hasira, mwenye kulipa kisasi na sasa amechukua hatua ya kikatili kwa mwanamume na mwanamke kwa yale aliyoyafanya. Hebu tuchukue simulizi tena katika mstari wa 14. Kwanza, Mungu anaiambia nyoka. Anasema, "kwakuwa

_______________________________________________________________________________

_______________________________________________________________________________…"

Mapambano yananza! Vita inaendelea. Sehemu zilizo chaguliwa zimewekwa wazi. Vita ni kati ya Mungu na mwovu. Kila timu ina hodari wake. Hawa ni aki na nani?

• Zaburi106:inatuambia kuwa mshindi wa milele ni?

_______________________________________________________________

1 Wakorintho15:57 kwa uwazi inasema kuwa Mungu ndiye mshindi!

_______________________________________________________________

• Waefeso 6:11-13 inatumia lugha ya picha kuelezea juu ya vita na mavazi ya kinga ya mishale. Nani mshindi wa uovu?

________________________________________________

Pigia mstari maneno katika mistari hii inayo elezea timu yake “dunia yake ya giza”

**FUNDISHO:**

Maandiko yote ni juu ya vita hivi na hasira yake kwa ulimwengu wa sasa. Biblia ni kitabu juu ya vita na upendo ambao ni dawa ya dhambi. Vitabu vyote lengo lake kuu ni kuhusu mada hii kuu. Wahusika juu ya mada hizi wame fafanuliwa. Mbinu zimewekwa wazi na mipango imefunuliwa. Jasiri ameshindwa. Habari inaanzia katika Mwanzo 3 na maneno ambayo Mungu aliimbia nyoka, “kwakuwa umefanya hivi”Hatimaye laana hii iliyosemwa na Mungu kwenye mistari inayofuata, mistari ya 14 na 15, anatamka kwa uwazi kile kinacho kwenda kutokea kwenye uhodari wa mwovu. Kwa ukweli, Ufunuo 12:9 inasemea juu ya mwisho wake pamoja na kundi la wafuasi wake wa uovu, “dunia ya giza”. Andika mstari huu:

_______________________________________________________________

_______________________________________________________________

_______________________________________________________________

Kwa hiyo, ugonvi unahusu nini? Mungu ni mwema na vyote alivyoviumba (Mwanzo 1:31). Makusudi yake ni kwamba watu alio waumba wafahamu mema ,na waishi katika uhusiano nay eye, wakiitikia Neno lake, Neno la yule ambaye ni Mwema. Lakini, kumbuka jaribu liloletwa na nyoka, ilikuwa ni kwamba wajue mema *na* mabaya. Aliwataka wawe upande wake. Aliwataka watii neno lake. Majaribu yake yalikwenda hadi kwenye kiini cha kuishi kwao. Wamepaswa kujibu swali: Nani angetawala ndani ya maisha na mioyo yao? Vita sasa ina hasira na roho ya mwanadamu. Mungu angeshinda au shetani angeshinda? Mungu hakukukusudia wajibu swali hilo. Aliwataka wampende na kumfanya atawale kwenye maisha yao.

Katika mstari wa 14 na 15 hasira ya Mungu inamwagwa kwa nyoka, katika uovu. Anaweka laana kwa nyoka, kwenye uovu. Yote ni maneno yanayo tumika kumaanisha shetani ambaye wakati mwingine anaitwa kama malaika aliyeanguka.

Mstari wa 14 na 15 inaongelea mwisho wake.

- Ame *laaniwa* na Mungu (mstari wa14).
- Atatembea kwa *kutambaa* kwa tumbo lake katika maisha yake yote. (mstari 14).
- Kichwa chake kitapondwa (mstari wa 15).

**KUCHIMBA KWA KINA:**

Mstari wa 14 na15 ni mistari migumu kueleweka, lakini ni muhimu kufahamu kuwa mstariwa 15 ni mstari wa kwanza katika Biblia unao ongelea ahadi ya kwanza ya Mungu ya kukomboa mwanadamu. (Kumbuka:Kuwa na uhakika kurudia maana katika somo la 2.) Mstari huu unaahidi kuwa Mungu atarejesha uhusiano uliovunjika ambao hata

sasa utengano huo upo na unatenganisha wanadamu wote, ki ukweli unatenganisha Mungu na viumbe vingine vyote. Matokeo ya uadui huu ambao upo kati ya nyoka na uzao wa mwanamke utakuwa ni nini?

- “Atakuponda kichwa” anaongelea ushindi ambao ni wetu, na ufufuo wa Yesu kama unavyo wekwa wazi kwenye Injili ambao tutaona kwa ufupi baadae kwenye vitabu vinne vya Agano Jipya. Pamoja na hayo kwa wale wanopenda kusomba zaidi kujifunza kuhusu kishindo cha kuponda, soma 1Wakorintho 15:20-28, 57.
- “…na utamuuma kisigino” fanya rejea kwa kifo cha Yesu. Kishindo cha kufa kwake, lakini ufufuo wake ni ushindi juu ya mwovu, “kuponda” kichwa.

**KUKARIRI:**

Kutambua Mwanzo kuwa 3:15 ni kifungu kigumu, pamoja na hayo, unatiwa moyo kukikariri. Mstari huu pamoja na mistari mingine, utakayo kusanya kupitia masomo haya yote, yatakupatia ufahamu wa kukaribia kadiri Mungu atakavyo endelea kufunua kwako habari ya ukombozi wako kupitia Neno lake. Andika Mwanzo3:15, kwenye kitabu chako cha rejea na ukariri mstari huu. “Ahadi ya Mungu” kwenye kitabu chako kina kukumbusha juu  ya ahadi ya Mungu ya kwanza ya kutukomboa wewe na mimi, na kutufanya kwa upya, watoto wake wa thamani.

## SOMO LA TATU ~~ SEHEMU YA 22

**ZOEZI:**

Matokeo ya dhambi yanaingilia uumbaji wote. Hii inaonekana kwa maneno ya Mungu kwa Eva katika mstari wa 16. Matokeo mawili ya dhambi yako wazi kwa mwanamke. Mungu alisema kuwa, matikeo yangekuwa nini?

1. Nitaweka
_______________________________________________________
2. Tamaa
________________________________________________________
Mwanamume pia naye aliasi. Maisha ya mwanamume pia yaliathiriwa na laana ya dhambi. Kutokana na dhambi Mungu alisema kuwa kungetokea nini?
1. "Laana ni
__________________________________________________________
_______"
2. "…kwa maumivu
__________________________________________________________
_______"
3. "kitatoa
__________________________________________________________
_______"
4. "…na wewe
__________________________________________________________
_______"
5. "…hadi
__________________________________________________________
________
__________________________________________________________
_______"

**FUNDISHO:**

Dhambi imefanyika. Mwovu amewekwa wazi na kufahamika yeye ni nani. Macho ya mwanamume na mwanamke yamefumbuliwa wazi na wanaona bayana. Dhambi si tukio la mara moja tu bali imepenya katika maisha yote, na itakuwa sehemu ya kuishi kwao hadi kufa. Ilikuwa ikifananaje? Labda kufahamu ukweli huu kwa karibu itakuwa ni vizuri

tukikumbuka wakati tuliposema, “Nisinge …”na baadae tunajikuta tukihuzunika kwa kukiri uhiari wetu wa kutenda matendo ya kutotii. Picha halisi ni pale mzazi anaposhuhudia kwa maumivu, matokeo matendo ya kutotii kwa mtoto wake. Hatua ya nidhamu inawezekana ikawa fursa iliyopotea, au ombi lililo kanwa, au adhabu nyingine inayo tolewa kama matokeo ya vitendo vya uasi au kutotii. Tumekuwa tukisikia ikisemwa kuwa “hii huniumiza sana,
au zaidi ya inavyo niumiza”
Mzazi hubeba mzigo wa matokeo yanayo telewa kwa mtoto.

**MAZOEZI:**

Lakini, Mungu alikataa kuacha peke yao Adamu na Eva, hata katika hali kama hii. Badala yake inaonekana akiwajali wale anaowapenda, wakati huu akiwatazama huku wakitumikia matokeo ya dhambi. Mambo matatu yanatokea kwa haraka na kila moja linaanzishwa na Mungu.
1. Kumbuka mstari wa 7 ili kufunika uchi wao waliunganisha majani ya miti. Ni jambo gani Mungu alifanya katika mstari wa 21?

____________________________________________________________________________________

____________________________________________________________________________________

Ili mavazi ya kudumu yatengenezwe, damu ya mnyama ilibidi imwagike. Kwa rejea ya kipindi kijacho ni vizuri kukumbuka tena kwamba kila habari yoyote ihusianayo na kufunika dhambi hudai sadaka, ya kumwaga damu. Kwahiyo, Waebrania 9:22 hutukumbusha kuwa kuwa “pasipo kumwaga

____________________________________________________________________________________

___________________________________________________________________________________”

2. Tatizo lilikuwa ni nini (mstari wa22)?

_______________________________________________________________
________

Kwanini alitakiwa  kuwazuilia mti wa uzima?

_______________________________________________________________
________

_______________________________________________________________
________

Kwanini alipaswa kufanya?

_______________________________________________________________
________

3. Aliweka nini mbele ya bustani?

_______________________________________________________________
________

Kwanini malaika, au maserafi aliwekwa hapo?

_______________________________________________________________
________

**MASWALI YA KUTAFAKARI:**

Chukua muda kukumbuka jinsi Mungu anavyo onyesha upendo wake kwa mwanamume na mwanamke, kupitia mawazo haya matatu. Andika tafakari yako kwenye daftari yako.

1. Je kulikuwa na jema lolote katika hali ya mwanamume na mwanamke kujaribu kujifunika aibu yao?
2. Je ingetokea nini kama wangekula mti huo, mti wa uzima wakaishi milele katika hali yao ya dhambi pasipo tumaini lolote la kurejesha uhusiano wao na Mungu?
3. Kwa kutambua tabia yao ya dhambi kumbuka upendo wa Mungu alio uonyesha kwa kuweka mlizi kwenye lango la bustani.

**SALA:**

Ee, Bwana Mungu, pamoja na dhambi zetu bado umeamua kutupenda. Hata kama tunashindwa kutii, na kuasi mapenzi yako na njia yako, unaendelea kuonyesha upendo na kujali viumbe vyote. Neno lako ni kweli. Unasema katika Warumi 8:39 kuwa "hakuna kinachoweza kututenga na upendo wa Mungu katika Kristo Yesu Bwana wetu" Asante kwa habari hii njema ya neema yako.

______________________________________________________________
_______________
______________________________________________________________
_______________
______________________________________________________________
_______________

## MAWAZO YA KUFUNGA SEHEMU YA 2:

Katika hatua hii katika masomo yako ya Mwanzo 3, Umemaliza mafundisho ambayo yanaweza kuibua maswali mengi kwenye fikra zako. Hatuwezi kusema kuwa, kila kitu kitafundishwa kwa upana kwenye somo fupi. Pamoja na hayo, ukweli wa muhimu kwako ni kuanza kufahamu Mungu, kama Mungu wa upendo, anaye kupenda kwa "upendo wa milele"(Yeremia 31:3); na kama Mungu mtakatifu ambaye husema "Kuweni watakatifu, kama vile Mungu wenu wa mbinguni alivo mtakatifu." (Matthayo 5:48).

Kama Mungu mtakatifu, hawezi kushirikiana na dhambi au kusamehe dhambi kwa kuipuuzia. Kama mtokeo, Anasimama katika upendo ili aokoe wanadamu kwa kuharibu dhambi ambayo humtenganisha na wale Anao wapenda, kusaidia mwanadamu kutoka katika mauti ambayo inaweza kututenganisha na Yeye, na kututoa kwa shetani, mwanzilishi wa dhambi.

Biblia ni habari juu ya Mungu jinsi alivyoamua kukomboa watu wake na kuwaleta kwenye uhushiano wa upendo pamoja naye  kwa mara nyingine. Haitendi kazi hiyo peke yeke, bali alichagua kutumia watu, historian a matukio mbalimbali, ili kutimiza ahadi yake aliyoifanya na Adamu na Eva katika bustani, kuponda adui na kurudisha uumbaji wote na kurejesha mahusiano na Yeye tena.

Makusudi yake ni kila mmoja wetu kumjua kwa ukaribu kama yeye aliyetupenda kwa kuja katika uhusiano wa mtu binafsi pamoja baye kupitia jina Mwana wake Yesu Christo kama mwokozi wa maisha yetu.

## SOMO LA TATU ~~SEHEMU YA 33

**UTANGULIZI:**

Adamu na Eva sasa wametolewa na Mungu kutoka kwenye Bustani ya Edeni. Tunaweza kuhisi jinsi walivyokuwa wakitembea kutoka bustanini wakiona ule upanga wa moto wa makerubi "ukizunguka ukilinda mti wa uzima."  Hii ni picha ya kutisha na kusikitisha. Hakukuwa na jinsi ya kuwasaidia, lakini wasiwasi ulijaa mioyoni mwao, wasijue maisha yatakayofuata.

Walikuwa hawajaishi maisha nje ya bustani. Walikuwa hawajajua kuishi maisha ya kujitegemea wenyewe. Walikuwa wakipewa kila kitu, kazi yao ilikuwa ni kufurahia uumbaji wa Mungu bustanini.  Kulikuwa na amani kati yao na viumbe vyote, maisha yangekuwaje Adamu atakapo anza kuvuna matunda kutoka kwenye ardhi ambayo ingetoa miiba na michongoma.

Eva alikuwa hafahamu lolote juu ya uchungu wa kuzaa wala ufahamu juu yamme wake kumtawala. Na Mungu alikuwa wapi sasa? Kwa mara ya kwanza, wanakabiliana na matatizo ya upweke. Japokuwa walikuwa pamoja katika ndoa, dhambi ilileta utengano katika mahusiano yao, jambo ambalo lilikuwa ni jipya kwao. Tunaweza kukumbuka maneno kutoka Mwanzo 2:24, "Wawili watakuwa mwili mmoja" zaidi ya hayo uhusiano wao na Mungu ulibadilika. Dhambi ilileta aibu na hatia ambayo iliwatenga na Mungu. Walijificha uso wa Mungu na kujichana wao kwa wao.

Habari inazidi kuwa mbaya tunapojifunza jinsi dhambi inavyo haribu uhusiano na ushirikiano kwenye familia. Soma Mwanzo 4.Mambo mengi hayajaandikwa kwenye sura hii. Ki ukweli somo la sehemu hii ya Mwanzo litakapo kamilika, utakuwa na maswali mengi kuliko majibu. Makusudi ya suru hizi za kwanza za Mwanzo ni kuweka wazi uharibifu wa mwovu na dhambi na mwanadamu alivyohusiana na Mungu, na wengine na uumbaji. Inafunua silaha za adui na nguvu ya kujeruhi, kutenganisha, na kuharibu. Tukiwa na haya katika mawazo hebu tuendelee.

Sura ya 4 inaweka wazi machungu ya dhambi kadiri inapozidi kupenya kwenye maisha ya familia. Hii inavyofunuliwa, tunahitaji kuona uwepo wa Mungu na anavyoingilia akiwa ni mwenye rehema na anayedumisha uumbaji wake.

**ZOEZI:**

Wahusika katika habari ya kitabu cha Mwanzo, kwa ghafla hubadilika kwa maneno, "Adamu akalala na mke wake….". Majina ya wana wake wawili ni yapi?

____________________________________na

_________________________________

Tunajifunza nini kuhusu kazi ya hawa watoto wawili (mstari 2)?

• Kuhusu Abeli?

_______________________________________________________

• Kuhusu Kaini?

_______________________________________________________

“Katika majira hayo” Kaini na Abeli walileta sadaka zao kwa Bwana Kila mmoja alileta nini?

• Kaini alileta

________________________________________________________

• Abeli alileta

_______________________________________________________

Ni itikio gani la Mungu kwa sadaka?

• Kwa sadaka ya Abeli

___________________________________________________

• Kwa sadaka ya Kaini

___________________________________________________

Na, Kaini aliitikiaje kwa kutopokelewa kwa sadaka yake?

• __________________________________________________________ _________

• __________________________________________________________ _________

**FUNDISHO:**

Kwa mtazamo wa haraka, Bwana haonekani kutotenda haka kwa ndugu hawa wawili, na matokeo yake ana nekana kusababisha chuki kati yao. Hatufahamu kama Mungu  alikuwa ame waelimisha kuhusu sifa ya sadaka inayokubaliwa na Yeye. Tunafahamu kuwa mstari wa 4 unatuambia kuwa “Bwana alimtakabali Abeli na sadaka yake” Tena, sadaka yake ilikuwa ya aina gani kumfanya Abeli na sadaka yake ikubaliwe mbele za Bwana?

Tunafahamu baadhi ya mambo. Abel alileta sehemu nono. Ina maana kuwa damu ilibidi imwagwe, ili kupata hizo sehemu nono. Kumbuka katika masomo yetu ya Mwanzo 3:21 kwamba, Bwana aliona ni sawa kumvika Adamu na Eva kwa mavazi aliyotengeneza kutokana na ngozi ya mnyama; na ikumbukwe kuwa, ili kupata ngozi lazima damu imwagike. Japokuwa hatuambiwi kwenye mistari hii faida ya kumwaga damu, lakini katika sehemu nyingine za Biblia hutufundisha kuwa kumwaga damu; ilikuwa muhimu kwa ukombozi wa mwanadamu. Damu ndiyo iliyotumika kufunika dhambi.

Hii ni muhimu kufahamika kadiri tunavyoendelea mbele; maana miaka mingi, mingi sana baadae, pia damu ya Yesu ilimwagwa msalabani. Kumwaga damu yake ilikuwa ni dhabihu ya mwisho ambayo ilifunika dhambi za watu wote. Tutajifunza haya kwa undani zaidi kadiri tunavyoendelea.

## SOMO LA TATU ~~ SEHEMU YA 44

**ZOEZI:**

Kwahiyo, "Kaini alikasirika sana na uso wake ulikuwa umekunjamana." Kwasababu Bwaba hakutakabali sadaka ya Kaini, alijisikia kukataliwa yeye na sadaka yake. Bwana alikuja kwa Kaini na kumuuliza, kwanini amekasirika na kwanini uso wake umekunjamana.
Bwana anauliza nini baadae katika mastari wa 7?
"Kama uki ___
________________________________________________________________
_
________________________________________________________________
________________

______________________________________________________________________
______________?"
Tena inafuata
"usipo
______________________________________________________________________
_________
______________________________________________________________________
________________
______________________________________________________________________
________________
______________________________________________________________________
_______________"

Mstari huu unasikika sawa na "lakini" ambayo Mungu alisema bustanini katika Mwanzo 2:17?
Mungu, "Nani wanakwenda kutumika?" Dhambi haibakizi kizazi. Inarithishwa toka baba hadi mtoto. Mungu akitenda kwa upendo anakuja kwa Kaini na kusema, "Usiruhusu dhambi ikutawale"
Kutoka moyoni anamwambia Kaini kwamba Anampenda na anataka awe katika kiini cha maisha ye. Lakini mwovu ni katili. "Dhambi inakuotea mlangoni." Hii inaleta picha na ujumbe gani kwako?

______________________________________________________________________
________________
______________________________________________________________________
________________
______________________________________________________________________
________________

Ufunuo wa Yohana 3:20 inatoa picha ya Yesu kwenye milango ya mioyo yetu. Andika mstari huu.

______________________________________________________________________
________________
______________________________________________________________________
________________

__________________________________________________________________
_______________
Gundua tofauti katika mwelekeo/mkao.
• Dhambi __________________________________________ katika mlango wako (Mwanzo 4:7)
• Yesu ______________________________________ katika mlango (Ufunuo 3:20)
Yesu anangojea kukaribishwa mahali dhambi inakootea au inako gonga, ikisubiri kwa muda ili kuona kama inaweza kujipenyeza ndani na kufanya uharibifu wake. Soma tena mstari wa 8. Kaini aliichochea hasira yake akamwita Abeli uwandani. Huko akamshambulia ndugu yake akamuua.

Mauaji yameelezwa kwa wazi. Hakukuwa na utaalamu wowote uliotumiwa, Hakukuwa na ujanja, hakukutumiwa sayansi yoyote katika mauaji haya. Kaini alimshambulia Abeli na kumuua. Kilicho fuata ni nini? Nani alikuja kumkamata Kaini na kumuwajibisha kwa mauaji ya ndugu yake? Unagundua kuwa inaf anana na pale Bwana alipo wauliza Adamu na Eva, "mko wapi?" katika Mwanzo 3:9 baada ya kula tunda lililo katazwa. Sasa Bwana na Kaini wana majadiliano
Bwana anamuuliza Kaini:
__________________________________________________________________
_______________
Kaini anajibu:
__________________________________________________________________
_______________
Bwana anauliza:
__________________________________________________________________
_______________
Tumia muda ufungue tena Mwanzo 3. Mungu anauliza nini katika mstari wa 13?

________________________________________________________________
_______________
________________________________________________________________
_______________
Dhambi inaendelea kutengeneza njia yake ya uharibifu. Ndugu yake amefariki. Mauti ya binadamu yalikuwa hayajatokea kabla. Hii ilikuwa ni nini? Mungu akamshika kwa aajili ya kuwajibika kwa kumwaga damu ya ndugu yake. Kwa siku na umri wakati mtu anaweza kupata shida kusoma magazeti au kufungua luninga pasipo kukutana na matukio ya fujo na uharifu unaoishia na kifo, tumekufa ganzi na kuto thamini nafasi ya Mungu katika maisha yetu. Jambo linalofuata Mungu alilosema linaweka wazi kabisa.

"Sikiliza! __________________________________________ya ndugu yako_______________
________________________________________________________________
_______________
________________________________________________________________
_____________."

Uumbaji ambao Mungu alifanya ni wa thamani kwake, na Husikia kilio cha ampendaye kutoka ardhini (Mwanzo 3:10).

Mara nyingine tena, dhambi ina matokeo yake. Ni matokeo gani ambayo Mungu anatamka ambayo yatampata Kaini kwasababu ya kumuua ndugu yake (Mwanzo 4:11)?

- "Ume ________________________________________________________________
______"
- "Utakapofanya kazi ________________________________________________________________
______"
- "Utakuwa ________________________________________________________________
______"

45
Na, kazi za Kaini zime
"________________________________________________
________kuzaa."
Ardhi ileile alimo kuwa akiishi sasa ime laaniwa na itakuwa "haitoi matunda tena" kwa mahitaji yake.
Kaini alisema nini zaidi kuhusu adhabu yake (Mwanzo 4:14)?
• "Umenifukuza
________________________________________________
_______,"
• "nitakuwa
________________________________________________
_______;"
• "nitakuwa
________________________________________________
_______,"
• "na atakaye
________________________________________________
_______."
Kumbuka, Bwana anafanya nini kilicho fuatia katika mstari wa 15?
• Anasemaje?
"________________________________________________
______
________________________________________________
____."
• Bwana anafanyaje?
________________________________________________
______
*Kumbuka*: Hatufahamu hiyo ilikuwa ni alama gani, pamoja na hayo, kwa Kaini ilikuwa ni alama ya huruma ya Mungu ambayo ilionyesha kuwa hakuhitaji adhabu nyingine ila hasira ya Mungu.

**SOMO LA TATU ~~SEHEMU YA 55**

Mstari wa 16 unasema kuwa Kaini
"_____________________________________________________________
_______________
______________________________________________________________
____________."

Kwa mara nyingine tunaweza kukumbuka mwisho wa sura ya 3, na kama tulivyo ona Adamu na Eva wakiacha bustani ya Edeni, tunaona Kaini akiacha uwepo wa Mungu na kwenda kuishi katika nchi nyingine. Kwa ufupi, hebu tuangalie urithi wa Kaini na baadhi ya maendeleo ya uzao wake ulioletwa katika ulimwengu wa wakati ule. Mstari wa 17 unatuambia kuwa alizaa mtoto aliyemwita

______________________________________________________________
______________

Katika mstri ule ule tunajifunza kuwa Kaini alikuwa

________________________________________

na akaiita

_____________________________________________________baada ya mwanawake

Inafuata orodha ya ukoo wa Kaini.

• Mstari 20: Jabali, baba wa

______________________________________________________________
_______

• Mstari wa 21: Jabali, baba wa

______________________________________________________________
_______

• Mstari wa 22: Tubali-Kaini ambaye

______________________________________________________________
_______

*Kumbuka*: Inafurahisha kuona kuwa kujenga, kulima, na muziki vimeisha tajwa kuwa vinaanza katika utamaduni wa wakati ule. Tunaona katika mstari wa 25 na 26 uzao wa Adamu na Eva. Eva alimzaa ________________________________________________________________ _______________

Seti alikuwa na mtoto aliyetwa ____________________________________________________________

Kwa nyongeza, katika mstari wa 26 tunaona Mungu akihusiana na watu wake kadiri walivyoanza ku "_______________________________________________________________ _____________."

Hii inatufahamisha maisha ya ibada na sala ,walipoanza kuliitia jina lake.

**KUCHIMBA KWA KINA:**

Tukitumia rejea hebu tuangalie sehemu nyingine ya Biblia ambazo zinatupatia habari zaidi kuhusu Abeli.

Ukiangalia katika Mwanzo 4:2 Biblia yako inawezekana ikakupatia rejea zinazofuata neno "Abeli". Kama siyo mstari wa 2, angalia kwa ajiri ya rejea zinazo fuata na neno "sadaka"/dhabihu katika mstari wa 4. Kwenye kolamu ya rejea tafuta mstari unao fanana na herufi inayo fanana ambayo inafuata haya maneno mawili.

Inawezekana Waebrania 11:4 itaorodheshwa kama mojawapo, kama si rejea pekee. Waebrania 11 inajulikana kama "sura ya imani." Ukiangalia kwa haraka sura nzima utagundua kuwa baadhi ya mistari inaanza na neno "kwa imani". Aidha utagundua kuwa wahusika wa Biblia

wametajwa kwa majina. Kwamfano, katika mstari wa 7 Nuhu ametajwa. Mstari wa 8 Yakobo, Yusufu, Musa na wengine baadhi ya mababa wa zamani wametajwa kwa imani yao.

- **MAFAFANUZI:**

Katika Waebrania 1:1 tunaelezwa maana ya ***imani***. Imani ni

______________________________________________________________
________

______________________________________________________________
________

Ukiangalia katika mstari wa 4, Abeli ameorodheshwa kama mmoja mababa wa ambao wametajwa kwa imani yao. Mambo matatu yametajwa juu ya Abeli:

• Kwa imani

______________________________________________________________
________

• Kwa imani

______________________________________________________________
________

• Kwa imani

______________________________________________________________
________

Mstari huu unakupa tafakari gani katika kujifunza kwako juu ya habari ya Kaini na Abeli katika Mwanzo 4?

______________________________________________________________
_______________

______________________________________________________________
_______________

______________________________________________________________
_______________

**MASWALI YA MATUMIZI:**

Katika Mwanzo 4:9, Mungu anamuuliza Kaini swali, “Ndugu yako yuko wapi?” Ni aki na nani katika maisha yangu ninaweza kuwatambua kama ndugu zangu?”

____________________________________________________________________________________________________

Jibu la haraka la Kaini ni, “Mini ni mlinzi wa ndugu yangu?” Ni kwa namna gani niko tayari kuonyesha kuwa, ninajali na kuhusika kwa wale ambao nimetambua kuwa ni ndugu zangu?

____________________________________________________________________________________________________

Wakati mwingine, nikiulizwa juu ya ndugu yangu, kwa nini mimi pia nina paswa kukubali kuwa sifahamu?

__________________________________________________________________

**SALA:**

Bwan, ni rahisi kumnyoshea kidole Kaini na kumlaumu na kusema, “nisingeweza kufanya hivyo” Pamoja na hayo, ninafahamu kuwa mimi pia mara nyingi nina wakwaza na kuwaumiza wengina, kwa maneno yangu na matendo yangu. Nakusihi unisamehe na urejeshe uhusiano wangu na Wewe na wengine. Niwezeshe niweze kutenda kwa kuwajibika, kwa heshima, na kwa upendo kwa watu wengine kama vile unavyo kuwa ukinitendea kwa rehema na kwa upendo.

__________________________________________________________________
________________
__________________________________________________________________
________________
__________________________________________________________________
________________

## SOMO LA NNE ~~ SEHEMU YA 11

**INTRODUCTION**:

Katika Mwanzo 4:25-26 tunajifunza kuwa Adamu na Eva walipata mtoto mwingine aliyeitwa___________________. Seti pia alikuwa na mtoto aliyeitwa _____________________.

Sura ya 5 inaanza na marudio ya uumbaji wa mwanadamu kutoka Mwanzo 1, na tena mstari wa 3 unaendelea na habari mpya kabla ya kuelezea ukoo unaoanza na Adamu na familia yake. Katika sura hii utagundua miaka mingi ya kila mtu aliyo ishi. Takwimu hizi zinaweza kuibua maswali ya kufurahisha, na yenye changamoto kwa ajili yako. Andika maswa haya kwenye kitabu chako, na endelea na masomo yako. Hatutachukua muda mwingi kwenye sura hii, lakini tutahitaji umakini kwa baadhi ya maelezo yenye kufurahisha na yenye changamoto.

**MASWALI:**

Katika Mwazo 5:1 tunakumbushwa kuwa…

• Mungu aliumba mwanadamu kwa ____________________ ________
_________________.

Soma Mwanzo 1:27.

• Mungu aliwaumba _________________________na
_______________________.

• Na, aka __________________________________________.
(Mwanzo1:28)

• Walipokuwa wameumbwa akawaita
"________________________________".

Mwanzo 5:3 inafunua kitu tofauti kuliko mstari wa1ulivyotueleza.

• Mstari huu unasema nini kuhusu mtoto wa Adamu?
______________________________________________________________
_______

• Ulikuwaje mfano wa uzao wa Adamu, tofauti na mfano wa Mungu ambao alikusudia binadamu awe nao alipomuumba?
______________________________________________________________
_______

Tazama pia Mwanzo 1:26, 27.

• Sura ya mwanadamu haikufanana tena na ya Mungu. Matokeo ya dhambi yaliharibu sura ya Mungu kwa vizazi vyote vinavyokuja.

**ZOEZI:**

Tumia muda kuorodhesha majina yaliyotajwa kwenye sura hii kutoka Adamu hadi Nuhu kwa mfuatano wa kuzaliwa kwao, pamoja na miaka yao waliyoishi:

**Jina Miaka aliyoishi Jina miaka aliyoishi**

Adamu miaka 930

Seti Miaka
Nuhu tazama Mwazo 9:29.

**MASWALI:**

• Ni ukweli gani wa kufurahisha uliojifunza kuhusu Enoki katika mstari wa 21-24?

_______________________________________________________________
________

_______________________________________________________________
________

*Kumbuka:* Kwa habari ya nyongeza juu ya Enoki soma katika "sura ya imani" Waebrania 11:5-6. Alitambuliwa na Mungu kama "aliyempendeza Mungu" mstari wa 6, unatueleza nini tunachohitaji kuwa nacho ili kumpendeza Mungu? ___________________ Imani Amini kuwa Mungu anaishi na wale "wamtafutao kwa moyo" hujifunua kwao!

• Nani aliishi kwa miaka mingi zidi?

______________________________________________

Jina lake limezoeleka kwako?

• Lameki alisema nini kuhusu mtoto wake Nuhu katika Mwanzo 5:29?

_______________________________________________________________
________

_______________________________________________________________
________

• Je Mungu alilaani ardhi au ilipata laana kutokana na dhambi ? Rudia: Mwanzo 3:17-19.

• Ni aki na nani watoto watatu wa Nuhu waliotajwa katika mstari wa 32?

____________________________________,

__________________________________,

na
______________________________________________________________________

## SOMO LA NNE ~~ SEHEMU YA 22

**UTANGULIZI:**

Mwanzo 6, 7, na 8 inaelezea habari ya gharika. Pamoja na hayo, sura ya 6, inaanza na mistari minne ya matatizo. Neno Wanefili katiaka mstari wa 4, kwa mfano, ni vigumu kuelewa. Zaidi ya hayo, swali linaweza kuja kichwani mwako. Hawa watu walitoka wapi? Nani alimuoa nani? Sawa na mstari wa 5 kuna mengi ambayo ni vigumu kuyaelezea na kwa hiyo bado hayajaeleweka. Kutambua ukosefu wa maelezo na haja ya ufafanuzi, somo hili halikusudii kujbu maswali haya ila badala yake kukuzoesha na simulizi ambazo zitakupa ufahamu wa Neno la Mungu na tabia yake. Kumbuka, vita ipo kati ya Mungu na mwovu kwa nafsi za kila binadamu. Haja yake ya upendo ni kurejesha mahusiano na wote aliowaumba, wote waliojitenga naye kutokana na dhambi.

Hebu tuanze somo letu la gharika kwa kusoma Mwanzo 6:5 hadi Mwanzo 8:22.

**ZOEZI:**

Mstari wa 5 wa sura ya 6 unaonyesha picha ya kutisha. Bwana aliona nini? Andika maneno ya mistari hii

______________________________________________________________________

_________________________________________________________________
________________

Mistari hii inatumia maneno matatu kuelezea jinsi uovu wa mwanadamu unavyoenea kila mahali:

- _________________________________ tabia ya mawazo yake yalikuwa
- _______________________________________________________________
_____ maovu
- _______________________________________________________________
_ wakati.

Dhambi ilichafua uumbaji wote. Dhambi iliingilia moyo na mawazo ya mwanadamu. Kwahiyo mwanadamu alikuwa na nia mbaya badala ya nia njema. Mwanadamu akawa mwenye dhambi, dhambi iliingilia matendo yake yote. Hata matendo mema yaliingiliwa na dhambi kwasababu uhusiano wake na Mungu uliharibika. Waebrania 11:6 inasema, "Na pasipo imani haiwezekani kumpendeza Mungu, kwakuwa kila amjiaye yampasa kuamini kuwa yupo na Huwapa zawadi wale wamtafutao kwa moyo". Katika hali hii ya kuchafuka uovu huongezeka (Mwanzo 6:5). Nenda mbele hadi mstari wa 11. Ni maneno gani mengine yanatumika kuelezea hali ya siku?

_________________________________________________________________
________________
_________________________________________________________________
________________
_________________________________________________________________
________________

**MASWALI:**

Mstari wa 6 unaelezea nini kuhusu Mungu?

_________________________________________________________________
________________

Mungu alijuta kwa kumuumba mwanadamu na moyo wake ulikuwa umejaa maumivu. Mstari wa 7 unatwambia kuwa Aliamua?

**TAFAKARI:**

Mungu aliamua kuharibu kila chanye pumzi ya uhai. Kumbuka hali ilivyo kuwa Mungu alipo azimia kuangamiza vyote vyenye uhai, hata ndege wa angani, kwa mfano? Andika uchunguzi wako kwenye kitabi chako unapojaribu kuingia, kuchunguza moyo wa Mungu …

1. Hii ilikuwa ni kufunua hasira yake, mlipuko wa hasira yake?
2. Ingekuwaje kuwa na hazina yako nzuri, uumbaji amboa ulifanyika kuwa taswira yako ambayo huonyesha kinyume chako?
3. Kazi ya Mungu ya uumbaji ni endelevu. Watoto wanazaliwa; Mimea na wanyama vinazaliana.

Kungetokea nini kama asinge chukua hatua hiyo? Nguvu ya uovu peke yake inge tawala? Vitu vyote vilivyoumbwa vinge potea milele?

4. Kama mwanadamu huchagua kufanya uovu basi uovu hutawala. Mungu aliumba binadamu kwa makusudi ya kumdhihirisha Yeye na wema wake, siyo kujiunga na nguvu za mwovu na kuzitumikia. Nia yake ilikuwa maisha ya binadamu kujenga msingi wa maisha yake kwake Mungu na Neno lake. Alitaka waishi maisha ya kutojitegemea bali ya upendo na kumtegemea Yeye. Ni ni kilicho chukua nafasi ya Mungu na kuwa dira ya maisha yao ?

**MASWALI YA MATUMIZI:**

1. Kumbuka kuwa Mungu ni Mungu wa mahusiano. Matakwa yake yalikuwa ni kuishi katika mahuhusiano ya upendo na uumbaji wake. Uhusiano wako na Mungu ukoje? Unajisikiaje kuhusu fikra na upendo katika moyo wako? Tafakari na uandike mawazo yako kwenye kitabu chako.

2. Kumbuka wakati ulipojaribu kumwendea mtu juu ya uhusiano wa upendo baada ya tukio la kuachana kwa watu wanaopendana. Labda inahusiana na wewa kukataa upendo wa Mungu kupitia kwa mwingine. Je kulitokea nini katika mahusiano yenu baada ya hapo?

**SALA:**

Bwana Yesu, Ninakushukuru kwa nia yako ya kuwa na uhusiano na mimi. Unaendelea kunipenda na kunisamehe pasipo kujali yale ninayo Kutenda. Japokuwa wakati mwingine hufanya mabo kukukwaza, bado huniita kwa upendo na msamaha. Nifundishe kukupenda zaidi na kuelezea upendo wangu kwako, na kuishi na wengine kwa upendo.

______________________________________________________________
______________

______________________________________________________________
______________

## SOMO LA NNE ~~ SEHEMU YA 33

Tangu Adamu na Eva walipoanguka dhambini,historia ya mwanadamu imezidi kuwa mbaya zaidi. Baada ya muda mfupi wa habari ya anguko, tunasoma habari ya Kaini kumuua Abeli, baadae tunaona kuwa dunia inafikia hali ya kusikitisha kiasi cha Mungu aliyeumba mbingu na dunia,

anafikiria "kufutilia mbali mwanadamu……kutoka uso wa dunia". Hali ya uumbaji wa Mungu unaonekana kutofaa. Lakini baadae, katika mstari wa 8 inakuja dalili ya matumaini…..

**MASWALI:**

1. Mstari wa 8 unaleta matumaini kupitia mwanadamu aliyeitwa_____________________.
2. Ni maneno gani yanayotumika kumuelezea katika mstari wa 9? Angalia pia 7: 1:

- ___________________________________________________________
_____
- ___________________________________________________________
_____
- ___________________________________________________________
_____
- ___________________________________________________________
_____

3. Nuhu alikuwa na wana wawili (mstari wa 10):
______________________________________,
______________________________, na
______________________________

4. Mungu alimshirikisha mpango wake Nuhu. Anamwambia nini katika mistari ya 13, 17?
___________________________________________________________
________
___________________________________________________________
________
___________________________________________________________
________

5. Ingawa dunia imejaa fujo na ufisadi, Mungu Anataka kuangamiza wanadamu na dunia, lakini bado, Anaonyesha upendo wake mkuu kwa familia ya Nuhu. Nuhu anapewa agizo gani? (verse 14)

______________________________________________________________

6.Ni yapi maelekezo yake kwa Nuhu kwaajili ya kujenga Safina? (mstari wa 14-16)

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

7.Baada ya safina kutengenezwa, ilimpasa Nuhu kufanya nini? (verse 19-21)

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

8. Nuhu amejenga safina na Mungu anampa agizo la kuipakia. (Mwanzo. 7:1-
3) Anamwambia Nuhu kuwa baada ya juma moja mvua itaanza na itadumu kwa siku___________ na ___________ usiku (mstari 4). Na pia inaongeza, "Nita

______________________________________________________________

________________________________________________________________________________________

9. Tunajifunza juu ya imani ya Nuhu katika Mwanzo 6:22 na tena katika Mwanzo 7:5. Tunaambiwa nini?

________________________________________________________________________________________

**ZOEZI:**

Hiyo tofauti inakuwapo kati ya mwanadamu wa ulimwengu na mtu aitwaye Nuhu. Rudia Mwanzo 6:5 kupitia7:5. Ni maneno gani yanayo tumiaka kulinganisha Nuhu na binadamu wa ulimwengu?

**Nuhu watu ulimwenguni**

Walipata upendeleo dhambi

**MATUMIZI:**

• Unafikiri maisha yalikuwaje kwa Nuhu na familia yake wakati kipindi cha miaka ya kutengeneza safina?

________________________________________________________________________________________

________________________________________________________________________________________

• Unaweza kukumbuka wakati ulipo bezwa au kujaribiwa kutokana na na msimamo uliokuwa nao juu kile ulicho kiamini?

________________________________________________________________________________________

_______________________________________________________________________________________

• Kumbuka ni maneno gani yaliyosemwa na yale uliyofanyiwa. Kumbuka hisia zako kutokana na uchaguzi wako ambao hakuwa ukiungwa mkono na walio wengi.

_______________________________________________________________
_________
_______________________________________________________________
_________
_______________________________________________________________
_________

**KUCHIMBA KWA KINA:**

Bila shaka, Nuhu alionekana kama mjinga kwa kujenga jengo hili ambalo halikuwa la kawaida kwenye mazingira ya ukame, akielezea habari ya gharikia itakayokuja na madhara yatakayo tokea. Hata kama alionekana mjinga kwa wale ambao waliona kila kujifunza kulikuwa ni maovu muda wote, kitabu cha Waebrania 11:7-8 kinatueleza juu yake "Na _________________________Nuhu, wakati__________________ kuhusu
_________________________________________________, ndani takatifu
_______________ (tisha,tii) tengeneza ___________kwaajili ya
_______________
Familia yake. Kwa __________________
yeye__________________________
________________________ na alikuwa___________________ wa
________________________________ ambayo huja kwa
__________________."

Nuhu alikuwa mtu wa . Alitaadharishwa na Mungu" kwa mambo abayo yalikuwa hayajaonekana ." Alimwamini Mungu na kumtii. Tunatiwa moyo kuwa watu wenye kutendea kazi imani  kwa yale ambayo Neno la Mungu linatuambian na kuitika kwa kile Mungu anenalo..

**SALA:**

Ee,  Bwana Mungu, Ulisikitika kutokana na hali ya uumbaji. Wanadamu waliamua kufanya kinyume na mapenzi yako.  Pamoja ha hali hiyo, Nuhu, alipata rehema kwa sababu aliamini kwamba ulikuwapo na akaamini Neno lako kuwa kweli. Nipe imani kama ya Nuhu ambayo inaamini Neno lako na mapenzi yako na kuyatii.

______________________________________________________________________
______________

______________________________________________________________________
______________

______________________________________________________________________
______________

## SOMO LA NNE ~~ SEHEMU YA 44

Safina inapakiwa.Mungu anafunga malango.Na mvua inanyesha kwa siku________ na _________
usiku! (Mwanzo7:17) Hebu tuone simulizi inasema nini katika sura ya 7…

**MASWALI:**

- Nani aliingia kwenye safina kufuatana na  mstari wa 7na 13?

______________________________________________________________________
________

______________________________________________________________________
________

- Ni wanyama gani waliojumuishwa? Angalia mistari  8-9, 14-15.

______________________________________________________________________
________

______________________________________________________________________

________

- Ni nani aliyefunga mlango baada ya kuona kila kitu kiko ndani? (msitari 16b)

______________________________________________________________________

________

- Ni maneno gani yanayo elezea gharika? (mistari11-12, 17-20)

______________________________________________________________________

________

______________________________________________________________________

________

- Ni nini vilivyo angamizwa?

o (masitari 21) –Kila chenye uhai…

______________________________________________________________________

__

o (msitari 22) –Kila kitu…

______________________________________________________________________

__

o (msitari 23) –kila chenye uhai…

______________________________________________________________________

__

- Ni kwa muda gani dunia ilifunikwa na maji? (mstari 24)

______________________________________________________________________

________

**TAFAKARI:**

Ni vigumu kubashiri ni mambo gani Nuhu na familia yake walikuwa wakifikiria wakata wa siku hizi za gharika na maangamizi. Hukumu ya Mungu juu ya wale waliokuwa hawana uhusiano naye, na badala yake waliochagua fujo na ufisadi ilikuwa ni mauti kwao. Nuhu alifahamu kuwa majirani zake, wafanya biashara wenzake, wana ndugu na ukoo

wake na jamaa zake alioishi nao siku zote, wate waliangamia. Mtu yeyote anaweza kufikiria hali ya kutisha iliyokuwa nje ya safina, lakini wakati huo huo, tambua amani na salama ambao Mungu aliwapatia humo ndani ya safina.

Nuhu na familia yake walikuwa hawajaambiwa na Mungu ni kwa kipindi gani wangeishi kwenye safina. Walifhamu kuwa Mungu anakwenda "kuleta maji ya gharika duniani ili kuangamiza vitu vyote vilivyo chini ya mbingu". Bila shaka, walikuwa wakisikia mvua ikipiga juu ya safina, Walijua kuwa siku 40, usiku na mchana mvua ilikoma. Lakini sasa, ni siku 150 baadae na safina inaendelea kuelea juu ya maji. Hapa ndipo Mwanzo 8 inapoanzia.

**ZOEZI**:
Ingawa Nuhu hakujua ni kwa muda gani wangekuwa kwenye safina, alijua yule aliyewahifadhi na kuwapa maitaji familia yake. Andika maneno matatu ya Mwanzo 8:1.

---

Mungu alimkumbuka Nuhu na vyote vilivyokuwa kwenye safina. Alijali uumbaji wake. Aliweka mpango wa kuwaachilia likini alipaswa kufanya jambo kwanza.
.Mistari inayofuata inatuambia nini?

• Mstari wa 1:
______________________________________________________________
________

• Msitari wa 2:
______________________________________________________________
________

• Msitari wa 3:
______________________________________________________________
________

- Msitari wa 4:

______________________________________________________________________

__________

- Msitari wa 5:

______________________________________________________________________

__________

Mwisho safina ilitua juu yam lima. Soma mstari wa 6 hadi12. Nuhu alijuaje kuwa maji yamepungua na mwisho kukawa na nchi kavu?

______________________________________________________________________

_________________

______________________________________________________________________

_________________

______________________________________________________________________

_________________

Majuma kadhaa yalipita kabla ya kukauka kabisa. Baada ya hapo Mungu alimwamuru Nuhu ku

______________________________________________________________________

_________________

______________________________________________________________________

" (Mistari 15-16).

Wakati ulitimia kwa Nuhu na familia yake, na wanyama wote aliokuwa nao kutoka nje. Inafurahisha kuwa maneno kutoka Mwanzo 1:28 yamesemwa kwa Nuhu katika mstari wa17. "…kwa hiyo yanaweza

______________________________________________________________________

_________________

______________________________________________________________________

_________________

______________________________________________________________________

______________."

**SALA:**

Bwana,asante kwa kunikumbuka. Kuna kipindi katika maisha yangu ninapo jihisi kusahauliwa na waengine, na kuwa mpweka. Maisha yangu yalionekana si ya thamani kwa wengine. Asante kwa kunikumbusha kuwa mimi ni wa thamani mbele yako.  Naomba maisha yangu yadhihirishe kukushukuru siku zang zote.

________________________________________________________________________________

________________________________________________________________________________

________________________________________________________________________________

________________________________________________________________________________

## SOMO LA NNE ~~ SEHEMU YA 55

**UTANGULIZI:**

Kwahiyo Nuhu alitoka kwenye safina, na kila mtu aliyekuwa pamoja naye. (Mwanzo8:18-19). Kama wewe ungekuwa ni Nuhu na ulikuwa umewekwa kwenye safina kwa miezi hiyo, unafikiri ni jambo gani la kwanza ungefanya? Ruhusu fikra zako kwenda!

________________________________________________________________________________

________________________________________________________________________________

________________________________________________________________________________

**MASWALI:**

Sasa safina ni tupu.Ni kitu gani cha kwanza Nuhu anafanya?

________________________

(msitari wa20) Nuhu anatengeneza madhabahu, na kutoa dhambihu ya kuteketeza kwa Bwana.  Tunajifunza kutokana na habari ya Kaini na Abeli kwamba, sadaka iliyompendeza Bwana ilikuwa ni ya mnyama kwaajili ya kumwaga damu Katika mstari wa 20, tunajifunza kuwa Nuhu alitoa sadaka ya baadhi ya ndege na wanyama walio kuwa kweye safina, ili kufanya dhabihu ya kuteketeza kwa Bwana. Angalia itikio la Bwna. Kwanza, Ali

_________________________________________

na akasema moyoni Mwake: “Hapana sitafanya tena

_____________________________________

kwasababu ya mwanadamu,

____________________________________________ kila

________________________________

ni_________________________________ toka

_____________________________.Na,

________________________________ nita

_______________________vyote_______________________________

___________, kama Nilivyo fanya

(msitari21)”

Ahadi yake inaendelea (mstari 22). Andika mistari hii…

__________________________________________________________

______________

__________________________________________________________

______________

__________________________________________________________

______________

__________________________________________________________

______________

**KUKARIRI:**

Ahadi hii ya Mungu katika Mwanzo 8:21-22 ni maneno mazuri sana ya kuweka kwenye kumbukumbu. Chukua muda uandike mistari katika kitabu chako, na jitahidi kukariri hizi ahadi kubwa. Unaweza kupanga mistari hii kama "ahadi nyingine ya Mungu"

**FUNDISHO:**

Mungu si kuwa hafahamu kutenda dhambi kwa mwanadamu. Lakini anasema kuwa, japokuwa anafahamu yale ambayo wanadamu watafanya na kuwa hali ya dunia itajazwa na fujo na ufisadi, pamoja na maovu ya kila aina, Anasema kuwa, hataangamiza tena viumbe vyote kama alivyofanya. Maneno "ingawa" ni maneno yanayodhihirisha huruma yake. Ni Mungu mwenye huruma.

- ***MAANA: Huruma*** **ina maana kuwa Mungu hakuamua kutufanyia kama itustahilivyo. Kutokana na dhambi zetu na hali a mioyo yetu ya kutenda dhambi, tunastahili kuadhibiwa na kufa. Katika Warumi 6:24 mshahara wa dhambi ni *mauti* lakini karama ya Mungu ni *uzima wa milele* katika Kristo Yesu Bwana wetu. Tunacho stahili ni kifo, lakini Mungu anatuonyesha Huruma yake kwa kutupatia kile tunachostahili.Badala yake, Anaonyesha upendo wake kwetu kwa kutupatia uzima wa milele katika Yesu.**

**MATUMIZI:**

Mfano unaoweza kukusaidia kuongeza uelewa wako juu ya rehema ni kuingia kwenye chumba cha maakama. Baadhi wamesimama mbele ya

jaji, wenye dhamira za uhalifu. Adhabua ni kifungo. Lakini mtoto wa jaji anasimama na kusema, “mheshimiwa, nitasimama kwa niaba ya huyu mtu.” Hatimaye yule jaji anamtangazia mhalifu “huna makosa” halafu anampeleka mtoto wake kifungoni. Adhabu imetekelezwa. Mtu ameachiliwa huru kwenda zake. Kesi imetupiliwa mbali.

Kwa mfano huu Mungu ni jaji. Sheria yake inadai haki itendeke. Malipo kwa makosa tuliyofanya lazima yalipwe. Tunasimama mbele za Mungu wanaoshitakiwa na dhambi zetu tunazo stahili ya kuadhibiwa. Mwana wake Yesu kwa vyovyote, alilipa dhambi zetu kwa kuchukua adhabu tuliyostahili sisi, katika nafsi yake. Kutokana na kuteswa kwake na kufa kwake, Mungu Baba anatangaza kuwa sisi kuwa “hatuna dhambi” Tumewekwa huru! Kesi imetupiliwa mbali. Fikiria kwa wakati fulani katika maisha yako; ni lini ulipofanyiwa huruma? Kulikuwapo hali gani?

______________________________________________________________

______________________________________________________________

Ulistahili nini?

______________________________________________________________

Badala yake ulipokea nini?

______________________________________________________________

Kumbuka mawazo yako na hisia zako ulipofhamu kuwa umepewa rehema..

______________________________________________________________

______________________________________________________________

**SALA:**

Mungu wa rehema na Baba, asante kwa rehema zako ambazo hunifanya kuishi kwa kuogopa kile ninacho stahili, lakini badala yake ninapokea kutoka kwako zawadi ya bure ya uzima wa milele. Asante kwaajili ya Yesu. Kama Nuhu, nipe imani ya kuona mkono wako wa rehema. Badala maovu kugandamiza moyo wangu, Umeamua kuwa hutaamgamiza tena, badala yake utaendeleza mpango wako wa uumbaji.

______________________________________________________________________________

______________________________________________________________________________

______________________________________________________________________________

**KUTAFAKARI:**

Mungu alitumia safina kuhifadhi masalia ya uumbaji wake. Safina ilitunza waliokuwamo, kwa usalama na walipita kwenye matatizo ya maji. Kumbuka katka maisha yako maisha yalipo onekana kusambaratika. Mahusiano yamekumbana na mashambulizi. Marafiki wanajikuta kwenye mazingira na hali ngumu kutokana na uchaguzi wao wa maisha yasio wa maadili mema. Labda wale mnaoshirikiana katika biashara wamekamatwa wakigushi au kuibia serikali, na matokeo yake sasa wanapambana na tishio la matokeo ya hali hiyo, na wengine kiasi cha kupoteaza ajira, kupoteza miji na hata familia.

Upendo wa Mungu unakuwa ni safina ambamo anatuinua juu ya kufikiri juu ya mahitaji na kupiga kelele kwaajili ya kutaka msaada. Mungu anahitaji wanadamu wote kwenye safina yake. Anataka tufahamu na

kupona huruma yake katika maisha yetu. Anataka tufurahie mahusiano yenye upendo pamoja naye, ambao unatufanya tuishi maisha huru kutokana na hofu ya mauti, na huru kufurahia maisha ya milele pamoja naye.

## SOMO LA TANO ~~SEHEMU YA 11

**UTANGULIZI:**

Katika somo la 4 tulijifunza juu ya habari ya Biblia kuhusana na gharika katika Mwanzo 6-8. Mungu alipoona uwezo wa maadili ya mwanadamu, fujo na ufisadi, dhambi na maovu, Aliamua kufuta kila kitu kutoka katika uso wa dunia, vyote vilivyokuwa na pumzi, wanadamu wote na wanyama. Alisikitikia hali ya dhambi ya uumbaji wake.

Mwanzo 6:8 inaanza, "Lakini Nuhu..." Kwasababu Mungu alimkumbuka Nuhu kuwa mtu mkamilifu aliyeishi katika mahusiano na Yeye, Mungu alishirikiana na Nuhu juu ya mpango wake wa kuangamiza, na akaagiza kutengenezwa kwa safina. Wakati safina ilipokamilika Mungu alimpa maelekezo Nuhu na mke wake kuingia kwenye safina. Zaidi ya hayo, kila aina ya mnyama kwa jinsia za kiume na kike, waliingia pamoja nao. Kisha Mungu alifunga mlango, na maji ya gharika yalishuka duniani. (7:10).

Maji yalipopungua kiasi cha kutosha, safina ilitua ardhini na waliokuwa ndani yake wakatoka nje. Katika mwisho wa Mwanzo 8, tulijfunza kuwa jambo la kwanza Nuhu alilofanya lilikuwa ni kutoa sadaka ya kuteketeza kwa Bwana. Hii ilimpendeza Mungu. Aliahidi kwamba "ingawa moyo wa mwanadamu ni muovu tangu utoto asingeangamiza tena viumbe vyote, kama alivyo fanya Sasa tuanzie pale tuliko ishia katika somo la 4 na Mwanzo 9.

Soma Mwanzo 9:1-7.
Mwanzo 9:1 inasikika kama marudio ya Mwanzo 1:26-28. Baraka iliyotolewa kwa mwanamume na mwanamke wa kwanza, sasa anampa Nuhu na watoto wake.
"Kuwa ___________________
na _______________________ ongezeka
__________________________dunia ."
Inasikika kana kwamba Nuhu ni Adamu mpya. Mungu yuko tayari kuanza tena, na anataka uumbaji wake kubarikiwa; kwa hiyo anawaambia "Mzaane na kuongezeka" Anataka "waijaze dunia". Hii ni baraka yake kwao.

**MASWALI:**

Anaendelea akiwaambia kuwa viumbe vyote katika nchi, bahari, na angani "wamepewa mikononi mwao". (msitari 2). Mungu anasema nini katika Mwanzo 1:26?

____________________________________________________________
_______________

Maelekezo kwa Adamu na Eva yalikuwa "tawala" viumbe vyote. Jambo lililofuata Mungu analosema katika Mwanzo 9:3 ni, "kila kitu

____________________________________________________________
_______________
____________________________________________________________
_____________."

Mungu anatoa nini kama chakula kwa uumbaji katika Mwanzo 1:29-31?

- Msitari 29 –Chakula kwa binadamu:

____________________________________________________________
________

- Msitari 30-31 – Chakuala kwa wanyama:

______________________________________________________________________________

Mungu anasema kuwa kila kitu kinacho ishi na kinacho tembea ni chakula kwaajili yao (Mwanzo 9:3). Lakini, mara nyingine, Mungu ameweke mashariti. Yalikuwa ni mashariti gani katika Mwanzo 2:17?

______________________________________________________________________________

______________________________________________________________________________

Ni mashariti gani kwa wakati huu katika Mwanzo 9:4?

______________________________________________________________________________

______________________________________________________________________________

**SALA:**

Bwana Mungu, Ulitoa kwa ukarimu kwaajiri ya uumbaji wako. Unatenda kwa huruma, hautuadhibu sawa na stahili yetu kwa maovu yote tuliyotenda. Badala yake ulichagua kwa ukarimu kumwaga upendo wako kwetu. Asante kwa baraka za kuzaa na kuongezeka na kuujaza ulimwengu. Unataka  dunia ijazwe na uzima. Unatupatia kwa makusudi na kwa malengo katika maisha yetu. Tufundishe kushika hizi Baraka takatifu za uzima.

______________________________________________________________________________

______________________________________________________________________________

______________________________________________________________________________

## SOMO LA TANO ~~ SEHEMU YA 22

**UTANGULIZI:**

Kwanini Mungu alisisitiza jambo hili katika Mwanzo 9:4 kwamba nyama haipaswi kuliwa, kwamba “bado ina uhai wa damu ndani yake” “bado ina uhai wa damu ndani yake?” Kitabu cha Mambo ya Walawi kina maana ya jambo hili, ambalo linaitwa sheria za kilawi. Hizi ni sheria za Mungu kwa watoto wake, wana wa Israel, au Waisrael, ambao wangeishi miaka mingi sana baadae katika historia ya ki-Biblia. Mambo ya Walawi 17:10-14 inatoa mawazo ya ndani kwanini Mungu alimwambia Nuhu karne kadhaa mapema kuwa nyama ambayo bado ina uhai wa damu haikupaswa kuliwa.

**KUCHIMBA KWA KINA: Soma Mambo ya Walawi17:10-14.**

• Ni thamani gani Mungu anaweka kwenye damu kufuatana na mistari hii?

______________________________________________________________
________

______________________________________________________________
________

Angalia hasa maneno katika mistari ya 11 na 14: “…_______________ ya kila

___________________________________

ni__________________________.”

Mungu anathamini damu kwasababu damu ni uhai wa kila kiumbe.
• Kwa nyogeza, Mungu ansema katika mstari 11 kwamba damu "hufanya ____________________________kwa ____________________________."
• Kabla ya uzima na kifo cha Yesu, wanyama walikuwa wakitolewa sadaka kwa Bwana kwa upatanisho kwa dhambi za wanadamu.Sadaka ya wanyama na damu iliyo mwagwa, ilituliza hasira ya Mungu kwa ajili ya wanadamu kutokana na dhambi zao. Mungu alikubali sadaka ya wanyama kama malipo ya dhambi zao, badala ya kufa kwa wanadamu. Damu ndiyo iliyofunika dhambi.

➢ ***MAANA*: *Dhabihu/sadaka* – Kutoa dhabihu kwa ajili ya dhambi za wanadamu ilimaanisha hakukuwa tena na chochote cha kuzuia au kuingilia uhusiano kati ya Mungu na mwanadamu. Ilimaanisha kuwa *walikuwa katika umoja* na Mungu. Damu liyomwagika ilichukuliwa kama sadaka ambayo ingeondoa dhambi za watu na kugeuza hasira ya Mungu. Mungu alisamehe dhambi za watu walipo mwaga damu ya wanyama na kumtolea sadaka.**

• Hebu tutumie sehemu nyingine ya maandiko kutusaidia kuelezea na kuelewa dhabihu/sadaka.
o Kutokana na Waebrania 9:22 tunajifunza kuwa "________________________ kumwaga ____________________________________ hakuna ___________________________________________________________.
o Warumi 3:25 inasema kuwa Mungu alitoa _______________________ kama mwisho________________________wa ________________________ na wote wamwaminio, kwa imani Huwahesabia haki (Chukua muda wa kurudia maana ya kuhesabiwa haki katika somo la 2). Sadaka ya mwisho ya Mwana wake, Yesu, ilileta mwisho wa sadaka nyingine, kwasababu

hakukuhitajiwa sadaka nyingine. Yesu alilipa gharama ya mwisho kwaajili ya dhambi kwa kumwaga damu yake msalabani badala yetu.

• Sadaka kwaajili ya dhambi za wanadamu iliendelea kusheherekewa katika historia ya maisha yote hadi wakati wa Yesu. Pamoja na hayo kufa kwake kulileta mwisho wa sadaka kwaajili ya dhambi; kwa sababu alikuwa ni dhabihu ambayo milele iliondoa dhambi za wanadamu wote. Kwa wale wanao amini kuwa dhambi zao zime samehewa, kwamba Mungu amewaweka *pamoja naye* milele.

**KARIRI:**

Katika sehemu hii ya somo, kuna mistari ambayo unashauriwa kuiweka kwenye kitabu chako na uikariri. Kumbuka kuandika rejea pale ambapo mistari inakutana.
1. Waebrania 9:22 – (kuanza) "…na pasipokumwaga damu hakuna masamaha wa dhaambi"
2. Mambo ya Walawi 17:11 – (mstari mzima)
3.Warumi 3:25 – "Mungu alimtoa kama sadaka ya upatanisho, kwa njia ya imani katika damu yake". Katika kila ukurasa wa kitabu chako kwa kila mstari andika maneno machache na vifungu ambavyo huleta kwenye mawazo, faida ya kumwaga damu.
Angalia somo na kifungu cha kila mstari kwaajili ya rejea za zinazo fuata
(i.e. Somo la 5 – Sehemu ya 2).

**SALA:**

Asante, Bwana Mungu, kwa kutenda kwa huruma yako, na kutotulipa sawa na stahili ya dhambi zetu, yaani mauti ya milele. Asante kwa kutupenda kwa kutupatia mwana wako Yesu kuwa sadaka ya utakaso,

ambaye aliondoa dhambi zetu, kutufanya “kutuweka pamoja” na wewe, milele.

________________________________________________________________________________

________________________________________________________________________________

________________________________________________________________________________

**SOMO LA TANO ~~ SEHEMU YA 33**

**UTANGULIZI:**

Tumetumia muda kiasi, kujifunza Neno la Mungu lililo semwa kwa Nuhu, na kwa hiyo limeimarika katika ufahamu wetu thamani aliyoipa damu. Unaanza kukariri mistari ya maana ambayo hujenga msingi wa kugundua thamani kadiri tunavyo endelea kujifunza. Mwanzo 9:5-6 imebeba sehemu ya nyongeza ya habari ambayo una ongeza thamani ya uelewa wetu kwanini Mungu ameweka thamani kubwa katika damu. Japokuwa inaweza kuonekana kama tunapoteza muda zaidi pasipo lazima katika somo hili; unatiwa moyo kusonga mbele.

Hivi visehemu katika mchakato wetu wa kukua kwetu katika kumfurahia Mungu, na kugundua thamani aliyotupatia na mahusiano anayotaka tuwe nayo tukiwa ni watu wake. Mungu alikuwa na msimamo juu ya uhai wa damu kwa kila mnyama na uhai wa damu kwa kila binadamu. Haishii kusisitiza kwamba nyama yeye damu isiliwa, lakini kapitia Mwanzo 9:5 Anaendele kusema kuwa
Ata ______________________________
_____________________________________ kutoka kila mnyama na mwanadamu.

**KUCHIMBA KWA KINA:**

Hebu kwanza tuangalie rejea nyingine ambayo huelezea kuhesabu uhai wa kila *mnyama*. Kama ilivyowekwa wazi kabla katika somo hili Mungu aliwapa watoto Waisraeli, sheria ya maadili walipokuwa jangwani miaka mingi baadae. Hizi sheria za kilawi zilielezewa kwa wazi. Alitaka waelewe kuwa zilitolewa kuwalinda kutoka tahari ambazo hazijulikani kwa hiyo zilitolewa kwajili ya kuwapa usalama na kuwahifadhi. Sheria ilikuwa ni njia ya kumtii Mungu na kumwitikia, kwa hiyo ilionyesha kuwa maisha ya watu wake yamejengwa katika Yeye na Neno lake pia. Hii ingeonyesha uhusiano wa upendo wanaoshirikiana naye. Katika Mwanzo 9:5 tunaelezwa kuwa "Atadai hesabu kwa kila mnyama." Ni upi mfano huu katika sheria zake zilizoandikwa katika Kutoka 21:28-32?

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

*Kumbuka:* DUsijali maelezo ambayo hayajaelezwa wazi kuhusiana na maelekezo haya. La msingi tafuta kuelewa nini Mungu anamaanisha katika Mwanzo 9:5 anapozungumzia juu ya "kudai haesabu kutoka kwa kila mnyama." Katika Mwanzo Mungu pia anasema kwamba kutoka kwa kila *binadamu "*Atadai ____________________________________ kwaajili ya ___________________________________________________________." Wakati ,mwingine kuhusika kwetu na uhai wa damu wa binadamu mwenzetu, unaonekana kutokuwapo. Kupitia vyombo vya habari tunaona mauaji ya kila siku. Luninga na maigizo yameondoa kujali thamani ya maisha na utu wetu. Mwanzo 9 inaweza kutulazimisha kuangalia haya yote katika mtazamo wa Mungu. Tunasikia Mungu akisema katika mstari wa 6, "Yeyote __________________________ ________________________

ya ____________________________,na
______________________________
_______________________________ita
_____________________________________.”
Kufuatana na mstari huu, uhai ulikuwa ni wa Mungu aliye utoa, na ni Mungu alipaswa kuuchukua. Kumbuka baraka za Mungu zilikuwa ni kwa ajili ya binadamu kushirikiana naye katika uumbaji. Aliwataka waongezeke na kujaza dunia, siyo kumwaga damu ya mwanadamu, au kudharau uhai ulio kwenye damu wa mtu mwingine. Mauti hudhihirisha dhambi, siyo baraka ya Mungu.

**KUTAFAKARI:**

Maneno haya yanaweza kuleta kwenye mawazo hali isiyo ya kawaida, na kuibua changamoto mbalimbali. Unaweza kujikuta ukishindana na mawazo mapya na haja ambazo hujawahi kuzifikiria kabla. Je haya mawazo mapya yanakusumbua? Zinakupa changamoto? Tumia muda kubainisha maswali: Mungu anasemaje? Je humaanisha yale asemayo?

• Ni kwa vipi ulimwengu wetu huonyesha utii wetu kwa kuitikia Neno lake?

____________________________________________________________
________
____________________________________________________________
________
____________________________________________________________
________

• Ni kwa jinsi gani ulimwengu wetu huonyesha kuto tii kwetu katika kuitikia Neno lake?

____________________________________________________________
________

______________________________________________________________________
__________
______________________________________________________________________
__________

• Maisha  tunayoishi ambayo yana tii Neno lake huonyesha ni yupi tuliye mchagua awe msingi wa maisha yetu.

o Maisha yangu huonyesha nini?

______________________________________________________________________
______
______________________________________________________________________
______

o Maisha ya rafiki yangu huonyesha nini?

______________________________________________________________________
______
______________________________________________________________________
______

o Ulimwengu wetu huonyesha nini?

______________________________________________________________________
______
______________________________________________________________________
______

**SALA:**

Nina mawazo na maswali mengi, Bwan. Katika somo hili nimekumbushawa kuwa Ulimbariki Nuhu kwa makusudi ya uumbaji wa maisha yake. Umemfanya kuwajibika kwa uhai wa damu wa binadamu mwenzake. Nifanye kuwa mlizi mwifadhi wa vitu na watu wengine kutokana na chochote kinachoweza kuwaondolea uhai wao.

______________________________________________________________________
_________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

## SOMO LA TANO ~~SEHEMJU YA 44

**FUNDISHO:**

Mungu alimuumba mwanadamu kwa mfano wake (Mwanzo1:27). Tunajifunza katika Mwanzo 5:3 kwamba uwezo wa mwanadamu wa kuonyesha ukamilifu wa mfano wa Mungu maishani mwake, uliharibiwa na dhambi. Watoto waliozaliwa na Adamu waliubwa kwa mfano wa Adamu. Japo aliharibiwa na dhambi, mwanadamu aliendelea kuwa na na sehemu ya mfano wa Mungu. Mungu hakutaka mwanadamu aliyekuwa na mfano wake achukuliwe na mwingine. Kumbuka lile Mungu alilo sema kwa Kaini katika Mwanzo 4:10 mara tu baada ya Kaini kuua ndugu yake Abeli, "Sikiliza! Damu ya ndugu yako inakulilia kutoka ardhini." Mwanzo 9:6 inasema, "kwa ____________________________wa ______________________

ali___________________________ ___________________________."

Mungu anaendelea kuweka thamani juu yetu tukiwa ni watu wanobeba mfano wake. Wakati damu ya mwanadamu inapomwagwa, yule anayebeba mfano wa Mungu anakufa. Kwakuwa tu wabebaji wa mfano wa Mungu, kwa sababu hiyo uhai una thamani kubwa kiasi hicho.

**MASWALI YA KUTAFAKARI NA MATUMIZI:**

Neno la Mungu husema kwamba, nimeumbwa kwa mfano wa Mungu. Wanadamu wenzangu pia wameumbwa kwa mfano wake. Maswali yameundwa kukusaidia kutafakari maana ya sisi kuumbwa katka mfano

wa Mungu, na kukumbuka thamani iliyowekwa katika maisha yetu binafsi na maisha ya watu wengine pia.

• Ni fikra gani zinakuja katika mawazo yako unapo kumbuka kuwa binadamu wote wameumbwa kwa mfano wa Mungu,  japokuwa uliharibiwa na dhambi?

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

• Je mfano wa Mungu unaweza kupotea? Vipi kuhusu wale wanaoweza kuchagua kumkana Mungu na kuishi maisha ya kujitenga naye?

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

• Ni thamani gani tunaweka kwenye maisha yetu tukiwa ni watu wanaobeba mfano wa Mungu? Maisha yako yanadhihirishaje thamani hiyo?

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

• Ni thamani gani unaweka katika maisha ya wengine ambao pia wanabeba thamani hiyo hiyo?

__________________________________________________________________________________________________________

__________________________________________________________________________________________________________

__________________________________________________________________________________________________________

Inawezekana haya yalikuwa maswali magumu kujibu, lakini isipokuwa tumetambua kuwa wote wameumbwa kwa mfono wa Mungu, tunaweza kusahau wajibu wetu wa kulinda na kujali wengine  - maisha yao yaleyale, mali zao, tabia zao, mienendo yao, na zaidi ya yote uhusiano wao na muumbaji wao.

**SALA:**

Ee Mungu , mara nyingi nimejifikiria mimi mwenyewe zaidi ya wengine. Nimeshindwa kuheshimu wengine kama inipasavyo. Sawa na mimi, wameumbwa kwa mfano wako, na uhai wao unatoka kwako. Mara nyingi ninasahau kuwa niko ndani ya Kristo na nimeitwa kukudhihirisha kwa viumbe wako, hasa kwa familia yangu, marafiki, na kwa wengine ambao wanaishi katika jamii moja na mimi.  Ni samehe ninaposhindwa, nisaidie nithamini uhai na kuwajibika kuulinda na kuutunza.

____________________________________________________________________________________________________________________

____________________________________________________________________________________________________________________

____________________________________________________________________________________________________________________

## SOMO LA TANO ~~ SEHEMU YA 55

**MARUDIO:**

Kabla ya kuendelea, hebu tuchukue muda kurudia rejea nne tulizojifunza somo lililopita. Mistari hii imefanya baadhi ya rejea kwa damu iliyomwagwa.

Ufahamu mpya juu ya upatanisho, kumwaga damu kwa ajili ya msamaha wa dhambi na uzima wa milele kwa wandamu, utaleta faida ya nyongeza katika vifungu hivi.

**Rejea**

**Faida ya mtu mmojammoja ya kumwaga damu**

Mwanzo 3:15 – Somo 3
Mwanzo 3:21 – Somo la 3
Mwanzo 4:8-11 –Lesson la 3
Mwanzo 8:20-21 –Somo la 4

**MARUDIO YA MAFUNDISHO:**

Tumetumia sehemu kubwa ya somo la 5 katika kukuza ufahamu wetu na kufurahia ukweli kwamba “uzima/uhai uko katika damu” na kwamba Mungu alituumba kubeba mfano wake. Mafundisho haya ya marudio yamekusudia kuonyesha picha ya umuhimu na upana wa umuhimu wa wa damu. Baada ya kujifunza hizi sura za kwanza za Mwanzo ni muhimu tukiunganisha baadhi ya hivi vipande kabla ya kuanza somo la 6, juu ya dhana ya Agano, ambayo imetajwa kwa mara ya kwanza katika Mwanzo 6:18. Hebu tutumie muda mfupi wa kurudia kwa kutumia rejea na maoni ambayo yatasaidia kuimarisha kujifunza kwako.

Hatutaanza kufhamu juu ya faida ambayo Mungu aliweka katiak damu, hadi tutakapo anza kufahamu lile Mungu alilomaanisha Aliposema katika Mwanzo 2:17, “kwa maana unatakapo lila utakufa hakika.” Haya

mauti ya dhambi yalikuwa mauti ya kuharibu umilele wote; kwasababu dhambi ilirithiwa toka kizazi hadi kizazi, hii ingekuwa hukumu ya wanadamu wote. Ni Mungu mtakatifu, na utakatifu wake ulidai gharama ya dhambi kulipwa. Isingepuuziwa au kusahauliwa; gharama ilipaswa ilipwe. Gharama ilikuwa ni kifo! Ukweli ni kwamba wanadamu hawawezi kujiokoa. Mwisho, gharama kulipwa ilitakiwa sadaka ya kifo cha Mwana wa Mungu, Yesu Kristo. Mungu alitoa ahadi ya Masihi. Katika Mwanzo3:15. Mungu aliwapa Adamu na Eva ahadi ya kwanza ya mwokozi. Alimwambia nyoka, “Nitaweka uaduhi kati yako na wanamke…A (Yesu) takuponda kichwa (shetani) na wewe (shetani) utamuuma (Yesu) kisigino.” Hiki kifungu kinaanisha kuteswa na kufa kwa Yesu, kumwaga damu yake msalabani. (Tazama Wakolosai 1:19, 20.)

Katika Mwazo 3:21 kabla ya Adamu na Eva kuacha Bustani ya Edeni Mungu aliwatengenezea mavazi ya ngozi badala ya mavazi waliyojitengenezea wenyewe, ambayo hayakuwa na kiwango. Damu ilitakiwa kumwagika ili waweze kuhifadhiwa na kufunikwa. Kitu fulani ilikipasa kufa kwasababu dhambi ilikuwa imeingilia uumbaji wa Mungu. Majani ya mitini na vichaka havikuweza kuwasetiri katika hali yao ya dhambi mbele za Mungu muumbaji wao.

Watu wote waliumbwa kwa makusudi ya kubeba mfano wa Mungu. Kubeba mfano wake ulikuwa ni dhamira na makusudi kwa upande wa Mungu, na alilichukulia kwa kumaanisha kabisa. Kwahiyo damu ya watu wote ni takatifu kwa Mungu na kwa sababu hiyo, kumwaga damu kwa mtu asiye na hatia hulia ikidai fidia, kama tunavyojifunza tunapoongelea Kaini mmoja aliyebeba mfano halisi wa Mungu na kwa kufanya hivyo Kaini hakudhihirisha mfano wa Mungu ambaye aliumbwa kwa mfano wake.

Tunajifunza katika Mwanzo 8:20 kwamba baada ya kila kitu kuacha safina kitu cha kwanza ambacho Nuhu alifanya ilikuwa ni kutoa sadaka kwaBwana. “Bwana alinusa harufu nzuri.” Hakukuwa na njia nyingine ingefanya huu uumbaji mpya ukubalike mbele za Mungu zaidi ya kumwaga damu. Kama ilivyo habari  katika Biblia nzima juu ya kazi ya Mungu ya ukombozi kwa ajili ya mwanadamu, katika hali zote rejea huwa ina uhusiano na kumwaga damu.

Aina nne za hali halisi tuliyorudia inajenga mazingira na msingi ambako rejea zitakazofuata zitakapoanzia. Uelewa wako utaongezeka kadiri utakavyoendelea kujifunza Neno la Mungu na kuanza kuelewa upendo wake wa ajabu kwetu.

**SALA:**

Katika hali ya marudio haya chukua nafasi ya kuandika sala yako mwenyewe. Kuja mbele zake, shirikiana naye katika shukrani na mawazo yako:

____________________________________________________________________________

____________________________________________________________________________

____________________________________________________________________________

____________________________________________________________________________

## SOMO LA IIX ~~ SEHEMU YA 11

**FUNDISHO:**

Katika somo la 5 – Sehemu ya 5 ilitajwa kuwa tungeelezwa juu ya wazo jingine jpya. Rejea ni Mwanzo 6:18. Mungu anashirikisha nia yake kwa Nuhu ya kuangamiza huai wote na kufanya agano na yeye. Andika mstari wa 18:

________________________________________________________________________________
_______________

________________________________________________________________________________
_______________

________________________________________________________________________________
_______________

Katika ahadi, Mungu anasema kwamba Anakwenda kuimarisha Agano lake na Nuhu.

➢ ***MAFAFANUZI: Agano* – Ni makubaliano yaliyoanzishwa na upande mmoja na kutolewa kwa upande wa pili. Agano huendelea kuwapo hadi upande mmojawapo huivunja au huacha mapatano. *Kumbuka:*Unaweza kuwa umezoea agano. Mfano, ukienda benki kwaajili ya kupata mkopo, benki huwa na wakala wa kuweka makubaliano kufuatana na mkopo na mkataba kwako mkopaji.Pande mbili zikisha saini, agano huwa walaka halali ambao utatumiwa kisheria. Kuhusiana na hali hii, Mungu aliazisha ahadi ya huruma yake. Ni ahadi ambayo anafanya,na hawezi kuivunja. Mungu anaimarisha agano na nani? (Mw10)**

1. ________________________________________________________________________________
_____

2. ________________________________________________________________________________
_____

3. ______________________________________________________________

Mungu huanzisha na huimarisha agano na Nuhu, watoto wake na kizazi kitakacho kuja. Anajumlisha na wanyama wote waliotoka ndani ya safina – na kila kiumbe kilicho duniani. Hii ni ya jumla, je' usingesema? Mwanzo 9:11 ni agano la kweli. Andika mstari huu.

______________________________________________________________
______________________________________________________________
______________________________________________________________

• Katika Mwanzo 8:21 Mungu aliponusa "harufu nzuri" ya sadaka ya Nuhu, unasema kuwa Yeye "alisema moyoni mwake…."Kutoka moyoni mwake, Mungu tunasikiia akisema kwamba hapana, Hataangamiza tena uumbaji kwa gharika. Shika sana matumizi ya neno "sitapiga tena" katika mwanzo 8:21 na Mwanzo 9:11. Ni mara ngapi Alitumia wao? _______________ Unawweza kumsikia Mungu akisema kwa sauti ya uamuzi, "Hapana, hapana, hapana tena..."

• Baadae, Mungu aliamua kutoa alama ya agano. Ilikuwa ni alama gani? ______________________________________________________________

• Soma mstari wa 12 na 13. Mungu alitumia upinde wa mvua kama alama kwetu, kwamba atakumbuka ahadi yake. Hutumia upinde wa mvua kama ukumbusho kwa ahadi yake ya huruma kwaajili ya viumbe vyote kwa vizazi vyote. Wakati wowote mawingu yanapotokea na upinde wa mvua hutokea na kusema "Nita ______________________________________agano langu." (Mwanzo 9:14-15)

• Inafurahisha kwamba, kila kunapokuwapo na upinde wa mvua swalil huwa linaulizwa: "Umeona upinde mzuri wa mvua?" Mara kadhaa huwa

tunaona pinde mbili za mvua. Tunaangalia kwa mshangao uumbaji wa Mungu unaoshangaza na ahadi yake "japokuwa…" (Mwanzo 8:21) "Hata…. tena (Mwanzo 9:15)

- Kwa mara nyingine tena anatumia maneno,

__________________________ katika mstari wa 15. Mara tano Anasema kwamba Hatatumia maji tena kuangamiza uumbaji. Mungu ni mwingi wa rehema kwa viumbe. Pasipo kujali hali yoyote itakayo vipata viumbe, hatupaswi kuogopa uharibifu wa jumla kwa maji ya gharika. Huruma yake kubwa huvumilia milele.

Katika mstasri wa 17 Mungu anasema "hili ni agano nililo weka." Hakuna sehemu ya agano hili iliyo mtegemea Nuhu, wana wake, viumbehai wala kizazi kilichofuata. Hii ilikuwa ikitegemea ahadi ya Mungu aliyotoa. Katika masomo yanayofuata tutajifunza juu ya maagano tofauti , ambayo Mungu aliweka pamoja na watu wake. Mengine yalikuwa na mashariti kama , "ukifanya hili" kwahiyo "Nitafanya hili." Walikuwa washike yote baraka na laana kufuatana na utii wa watu wa Mungu.Tuta angalia kuhusu haya maagano toafauti kwa upana zaidi, kama yalivyo wekwa. Kwa sasa ni vizuri kuelewa kuwa hili agano lililo wekwa na Mungu pamoja na Nuhu lilimtegemea Mungu ambaye aliahidi kuitunza kwa vizazi vyote.

**MATUMIZI:**

Mungu alisema Hataangamiza tena uhai wote kwa gharika.

1. Agano hili linaleta tofauti gani katika maisha yako?

____________________________________________________________
________

____________________________________________________________
________

2. Nikiamini kuwa Mungu aliahidi, kwa nini nina amini kuwa Atatunza ahadi yake?

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

3. Je, ni rahisi kwangu kuamini kuwa Hataruhusu gharika kama lile tena? Kwa sababu ninaon upinde wa mvua? Kwasababu…

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

4. Nina onyesha mfano wa Mungu katika maisha yangu kwa jinsi ninavyo weka na ninavyo tunza ahadi hizo kwa ajili ya watu wengine? Je wengine wananitengemea kwasababu wanajua kuwa niliyoahidi kufanya kuwa nitayafanya?

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

**SALA:**

Bwana Mungu, Umeanzisha agano lako kwa huruma pamoja na viumbe wote wenye uhai, ukiahidi kuwa hutatuma hasira yako na kuangamiza uumbaji kwa maji ya gharika tena. Umetunza ahahdi yako. Neno lako ni ukweli. Niwezeshe kukufuata kwa kupitia maneno niayosema. Wengine wafahamu kuwa yale ninayo yaahidi nitayatunza na kuyatekeleza na kwamba yaimarishwe kwa miaka yote. Asante kwa kuwa Neno lako linaweza kuaminika na kutupatia msingi ulio imara ambao juu yake ninaweza kujenga maisha yangu.

______________________________________________________________
_______________
______________________________________________________________
_______________
______________________________________________________________
_______________

## SOMO LA IIX ~~ SEHEMU YA 22

**UTANGULIZI:**

Tunakaribia kuacha habari za Nuhu na gharika, pamoja na hayo, kuna habari moja zaidi kumaliza. Mwanzo 9:18-19 inatoa baadhi ya mafundisho kuhusiana na wana watatu wa Nuhu ambao walitoka kwenye safina:

• Kwa marudio, majina yao ni aki na nani? ____________________,
__________________,
na_______________________________

• Ni jambo gani la kipekee limetajwa kuhusu Hamu?

______________________________________________________________
_______

• Mstari wa 19 unasema nini kuhusu hawa wana watatu?

______________________________________________________________
________
______________________________________________________________
________

Mengi zaidi yata semwa kuhusu hawa watu katika mistari inayofuata. Kwasasa pokea habari hizi tu. Soma Mwanzo 9:20-28.
Tunajifunza nini kuhusu Nuhu katika mstari wa 20?
1.

______________________________________________________________
________

2. ________________________________________________________________

Tunajua kuwa habari hii haitokei ghafla kwa kufuata gharika, tunajua kuwa inachukua miaka mzabibu kustwi Kuwa "mtu wa ardhi" alitoka nje kwenda kupanda mzabibu kutokana na tunda la zabibu alitengeneza divai na alikunywa kiasi cha kuwa mlevi. Mstari wa 21 unasema kuwa "ali lala ________________________________________________ ndani yake______________________________." Iwapo Nuhu alikuwa hana nguo kabisa, au alila akiwa wazi au bila kufunikwa hatufahamu. Hebu tufikirie yale tunayo yafahamu:

• Nani alimuona Nuhu kwanza?

____________________________________________________

• Aliona nini?

________________________________________________________

• Alifanya nini?

_________________________________________________________

Kwa vyovyote, kwa kawaida ya yanayo tokea, Nuhu alikuwa katika hali ya aibu, na mtoto wake Hamu ambaye alimuona kwanza, hakufanya lolote zaidi ya kuongelea jambo hilo kwa ndugu zake.

• Shemu na Yafeti walifanya nini?

________________________________________________________________

________________________________________________________________

• Hawa wanaume walifuata njia ndefu kwa kuhakikisha kuwa hawaoni aibu ya baba yao iliyokuwa wazi. Mstari wa 23 unasema

________________________________________________________________

• Nuhu alizinduka "kutoka kwenye divai yake" na kukuta vile Hamu, mtoto wake wa mwisho, alilolifanya. Anafanya nini?

________________________________________________________________
_________

• Kushindwa kwake kufunika aibu ya baba yake kulimsababishia matatizo. Alilaaniwa na baba yake. Ilikuwa ni laana gani kama ilivyoandikwa katika mstari wa 25?

________________________________________________________________
_________
________________________________________________________________
_________

• Nuhu alitoa baraka Shemu na Yafeti. Alisema kwa Shemu, “Imebarikiwa

________________________________________________________________
_________
________________________________________________________________
_________

Kwa Yafeti alisema,

________________________________________________________________
_________
________________________________________________________________
_________

**MATUMIZI:**

Jambo la heshima lilikuwa jambo la thamani kwa wale waliokuwa wakiishi chini ya agano jipya la Mungu, agano la rehema. Ni vigumu kuelewa jinsi kwa haraka katika historia matukio haya yalitokea. Mtoto wa Nuhu alimwaibisha baba yake. Hamu alimtendea baba yake mambo yasiyo ya heshima. Dhambi iliendelea kuacha alama yake katika familia za wazazi na watoto,  na wote wanaachwa na aibu na unajisi. Katika siku

hizi zetu, heshima kwa wazazi inazidi kupotea. Watoto huongea na kutendea wazazi na wakubwa kwa utovu wani dhamu hufanyika pasipo matokeo yoyote. Kwa baadhi ya watu mahusiano katika familia yamevunjika kabisa kiasi cha kuheshimiana kutokuwapo tena.

• Je unakubuka uliposhuhudia wazazi na wakubwa walipofanyiwa mabo yasiyo ya heshima? Labda ulihusika katika tukio hilo kwa njia moja au nyingine…

o Sababu ilikuwa ni nini?

___________________________________________

o Matokeo yalikuwa ni nini?

___________________________________________

• Kumbuka wakati tulipo kuwa tayari kwa makusudi kujaribu kulinda wengine badala ya kukimbia na kuambia wengine?

________________________________________________________

________

________________________________________________________

________

**SALA:**

Bwana Mungu, Ninakiri kuwa mara nyingi huongea na kuweka wazi mabo ya watu wengine badala ya kutafuta jinsi ya kuwafunika na kuwalinda. Nipe moyo ambao utachagua kulinda heshima na tabia za wengine. Asante kwa kufunika hali yangu ya aibu kwa damu ya Mwana wako, Yesu, Mwokozi wangu.

________________________________________________________

______________

________________________________________________________

______________

________________________________________________________

______________

## SOMO LA IIX ~~ SEHEMU YA 33

Mwanzo 10 imeandika habari ya ukoo wa watoto wa Nuhu. Kila habari imeandikwa katika 1Nyakati: 1. Unaweza kufurahia kufuatilia katika kitabu cha kwanza, cha Mambo ya Nyakati kama tunavyofanyia kazi Mwanzo. Habari hii itakuonyesha ustaarabu ulikoanzia baada ya gharika. Mwanzo 9:19 inasema kwamba "kutoka kwao walikuja watu ambao
_________________________________."

Hebu kwanza tuangalie Yafeti, mtoto wa kwanza wa Nuhu katika Mwanzo 10:1-5.

• Yafeti alikuwa na watoto wangapi?
_______________________________ (mstari wa 2)

• Msisitizo umewekwa kwa wana wawili na wana wao:

o Katika mstari wa 3:
_______________________________________________________

o Katika mstari wa 4:
_______________________________________________________

• Ni ukweli gani wa muhimu umeonyeshwa katika mstari wa 5?
____________________________________________________________
________
____________________________________________________________
________

• Inaweza kufurahisha kukumbuka kuwa familia ya Yafeti ilielikea Mashariki katika nchi za Asia Ndogo, inayojulikana sasa kama Uturuki, na Ulaya. Mistari ya 6-20 inaongelea juu ya watoto wa Hamu.

• Familia ya Hamu ilihamia sehemu inayojulikana sasa kama Israel, Afrika ya Kaskazini na Misri.

• Hamu alikuwa na wana wangapi?
________________________________ (mstari wa 6)

• Kushi alikuwa na wana watano. Mmoja wa wana wake ametajwa kipekee katika (mstari wa 8)
o Jina lake alikuwa nani?
_______________________________________________
o Mstari wa 8 unaweka habari gani za nyongeza?
____________________________________________________________
o Hakuwa jasiri wa vita tu, bali pia alikuwa
____________________________________________________________
o Iilisemwa neno kuhusu Nimrodi?
____________________________________________________________
o Mistari ya 10-12 inaongelea juu ya kukua kwa ufalme wa Nimrodi.
1. Babeli (mstari wa 10)
2. Ashuru (mstari 11)
3. Ninawi (mstari 11)

*Kumbuka:* Babeli na Ashuru ina kumbukumbu kubwa kwa taifa la Israeli. Babeli iliiteka Yuda na Ashuru iliteka Israeli. Waisraeli walishikiliwa kama watumwa katika nchi hizi kwa miaka mingi. Ninawi ulikuwa mji uliojengwa na Nimrodi. Kitabu cha Yona kinaeleza kilichotokea kutokana na Mungu kumtuma nabii asiye tayari katika nchi hiyo. Mengi kuhusu eneo hili, yataelezwa kwenye masomo yatakayo fuata.
• Majina mengine ya kutaja yaliyo kuwa ya muhimu katika historia ya Israeli.
o Wafilisti (mstari 13) wanaweza kuwa maadui wa Israeli waliodumu kwa muda mrefu katika historia ya Israeli wakati wa mfalme Daudi.
o Wakanaani (mistari 15-18) waliishi katika nchi ambayo Mungu alitoa kwa wana wa Israeli. Wana wa Israeli wanapokuja kumiliki nchi walikutana na mataifa katili: Wahiti, Wayebusi, Waamori, na Wahivite

kwa kutaja wachache tu. Kadiri uonavyo, hawa wote walikuwa ni uzao wa Nuhu ambao Nuhu alilaani.

o Koo za wakanaani zilitawanyika. Huu utakuwa ni muda muafaka wa wa kuangalia ramani nyuma ya Biblia yako. Inawezekana ramani itakayo kuwa ya msaada zaidi, ni ile inayoonyesha ufalme wa Israeli wakati wa utawala wa Mfalme Daudi a Sulemani. Jaribu kuonyesha miji hii na miliki zake:

• Sidoni – Kaskazini mwambao wa bahari ya Mediteraniani

• Gaza – Kusini, pia pwani

• Sodoma na Gomora – iko upande wa mashariki mwa bahari mfu. (unaweza kuhitaji kuitafuta kweye ramani ya kwanza.)

• Ufilisti – nchi ya Wafilisti

o Maeneo haya yanakupa utangulizi wa maeneo ambayo ni ya matukio muhimu katika historia. Pia unaangalizwa kuto katishwa tamaa na majina ya ajabu na mageni. Hii ni taarifa ambayo itakusaidia kufurahia alama za maeneo ya kihistoria.

Mistari 21-31 inaongelea juu ya wana wa Shemu. Huu ukoo wa Shemu ni wa muhimu sana katika historia ya Biblia. Huu ni ukoo wa mtu mmoja kama Abrahamu, Isaaka, Yakobo, Yusufu, Mfalme Daudi, na Mfalme Sulemani. Kwasasa tutaangalia yafuatayo:

• Uzao wa Shemu, mwana wa kati wa Nuhu, alihamia maeneo ya Kusini ambako kunaitwa Mesopotamia katika Biblia, na ambayo tunaifahamu kama Penunsura ya Pasia.

• Shemu alikuwa na wana wangapi?
________________________________ (mstari 2)

• Fungua katika 1 Nyakati 1:24-27. Kwa ufupi sana tunaambiwa kizazi kati ya Shemu na Abrahamu. Kamilisha chati hii ya koo.

.

**Shemu**

Abrahamu, huyu ni
Abrahamu

Onyesha haya majina kadiri uwezavyo katika Mwanzo 10. Zipigilie mistari

*Kumbuka:* Mtu anaweza kushangaa na hata kubishi juu ya umuhimu wa orodha ya vizazi kama hivi. Ukiangalia mbele katika Mwanzo 11 nyingine imeorodheshwa. Ingawa ukoo unaweza usionyeshe faida yoyote katika hatua hii, kama historia inavyo weka wazi. Ingawa watunza kumbukumbu za vizazi zinaweza kuonyesha kutokuwa na manufaa kwa sasa, lakini baadae tutaona kwamba kwa upande wa Mungu, kumbukumbu za za ukoo wa Nuhu ni muhimu sana, hata tukirudi nyuma katika kumbumbu za habari za ukoo wa Adamu.
.

**MATUMIZI:**

Uliisha fuatilia historia ya ukoo wako? Watu wengine huchukulia hili kwa makini sana. Kwa wengine hutumaini kuwa mtu fulani muhimu atapatikana kwenye mzizi wa ukoo wake. Chukua nafasi kukumbuka wale walio kutangulia. Kama ukiweza, ulizia familia yako juu ya hawa watu. Jifunze habari zilizohusianishwa na urithi wa familia yako. Huu unaweza kuwa wakati wa kumshukuru Mungu kwa ajili ya mtu fulani aliyefanya jambo la muhimu na la kukumbukwa katika maisha yako.

**SALA**:

____________________________________________________________
______________

____________________________________________________________
______________

____________________________________________________________
______________

____________________________________________________________
______________

____________________________________________________________
______________

Kuna ukoo mwingine ungependa kukumbuka.

• Ni aki na nani waliokuwa wazazi wako wa kiroho? Ni aki na nani walio kushirikisha imani yao, nani waliokuombea, na waliokuelekeza kwa Yesu? Labda wewe ulieleza habari za Yesu katika ukoo wako. Nani aliyeshirikiana nawe?

_______________________________________________________________

• Huu unaweza kuwa wakati wa kushukuru Bwana kwa ajili ya mtu yule ambaye alipenda wewe ujue habari za Mungu ambaye anakupenda na anakusamehe, Mungu ambaye hutenda kwa huruma kwa ajili yako, Mungu aliye kuumba na hutafuta awe na uhusiano na wewe milele.

**SALA:**

_______________________________________________________________

_______________________________________________________________

_______________________________________________________________

Na unaweza kuanza mzizi mpya kwa kumsaidia mtu kuanza upya safari ya maisha yake ya kiroho.

• Ni mtu gani ungeweza kumwelekeza kwa Mungu kupitia Neno lake?

_______________________________________________________________

• Huu unaweza kuwa wakati wa kumshukuru Mungu kwa wakati huo, kushirikisha upendo wake kwa wengine. Unaweza ukaamua kumuomba akupatie macho ya kuona wale ambao bado hawajamfahamu.

**SALA:**

______________________________________________________________________
________________
______________________________________________________________________
________________
______________________________________________________________________
________________

## SOMO LA IIX ~~SEHEMU YA 44

**FUNDISHO:**

Habari moja zaidi imebaki kaka sehemu hii. Inachukua nafasi Shinari au Babeli, ambayo ni Iraki ya sasa, katika nchi ya Mashariki ambako ukoo wa Hamu waliishi (Mwanzo 10:10). Habari hii inapatikana katika Mwanzo 11:1-9.

• Mstari wa 1 unasomeka,
“Sasa_______________________________________________ilikuwa mmoja
______________________ na
_____________________________________________.”

• Waliweka vichwa vyao pamoja na kusema, “Haya,
______________________________________________________________________
_________
______________________________________________________________________
_______.”

• Tunaambiwa kuwa walitumia
“__________________________________________badala ya
na _____________________________kwa
______________________________.” Hii ingeonyesha jamii iliyoendelea zaidi ambayo ilitengeneza vifaa vyao vya ujezi.

• Tena wakasema, “Haya, na ____________________________________ sisi wenyewe

_______________,na _________________________________ ili ifike
_________________________________________________________, ili kwamba
_______________________________________________
ili_________________ tawanyike
______________________________________________________.”

**MASWALI:**

Unaona tatizo hapa? Kulikuwa na ubaya wowote kwa yale yaliyopanga kuyakamilisha?

________________________________________________________________
______________

Je kuna mambo unaoyoona yakitokea katika kizazi hiki yanayofana na haya?

________________________________________________________________
_______________
________________________________________________________________
_______________

Kulikuwa na ubaya kwa kutumia tekinolojia waliyokuwa nayo kwa kujenga mji wenye mnara mrefu?

________________________________________________________________
_______________
________________________________________________________________
_______________

Lazima kulikuwa na shida fulani, pamoja na ukweli huo, kwasababu mstari wa 5 unaaza na neno moja kubwa:

________________________________________________________________
_______________

• Bwana anashuka kuangalia mradi wao wa ujenzi – mji na mnara waliokuwa wakijenga. Aliamua nini? (mstari 6) “Tazama

__________________ watu wanaongea __________________ language wame ____________________________, ______________________ hawata ______________________________________________.”

• Kwahiyo akasema, “Haya na tushuke, _______________________________ ___________________________ ___________________________ wasi ______________________________________________________ wao kwa wao.”

**FUNDISHO:**

Lugha yao moja iliwafanya wafanye nini? Kulitokea nini  katka fikra zao? Maono ya maisha yao yalikuwaje? _______________________________________________________________ _______________

• Waliambiana, “Haya na tufanye…” “Njoo na tujenge…” Tatizo ni kwamba walijifanya kiini cha maisha yao wenyewe: Haya hebu na *tujijengee* wenyewe mji”

• Hawakutaka kutawanyika. Walitaka kufanya uumbaji wao, kituo cha maisha yao. Lakini kuumba mji na mnara mrefu ambao “utafika mbinguni”walikusudia kujijengea jina. Watu na mataifa wangewajia. Walikusudia kuwa kituo cha anga yao.

• Walidhani kuwa wangetengeneza mnara ambao ungefika mbinguni. Kwa kufahamu  yale tunayo yafanya siku hizi kufuatana  na vurugu zilizo angani, jaribio lao linaonekana la kuchekesha. Unahisi ulimi mdogo katika mashavu kama Mungu asemavyo, “Na tushuke chini….”. Hakukuwa na njia nyingine ambayo mwanadamu angefika mbinguni.

• Mwamko wao wa ubinafsi kutumia maarifa yao, ustadi wao, elimu yao na uwezo wao wa kujitengenezea jina, vinalia vikihitaji kuwa macho. Wanaweza kufanya chochote watakacho wakiwasiliana kwa uhakika, pamoja na hayo, kama lugha yao ikivurugwa hawatakuwa tayari kuelewana,  na ubinafsi wao unge wafanya kusitisha mradi huo.

• Kwahiyo, Bwana alishuka (mstari 7) na akavuruga ______________________.
Hawakuweza tena kusikilizana. Kwa hiyo, kwa mfano kama mjenzi angeulizia nyundo, angepewa pisipisi.
• Jambo lile walilotaka—kutotawanyika—hilo ndilo jambo Bwana alilofanya. Mstari wa 8 unasema, "Basi Bwana _______________________ kutoka _____________________ nchi yote.
• Na ujenzi wa mji ukasitishwa. Haikucheleweshwa wakati kila mtu alikwenda kufuatana na kundi makundi ya lugha. Hapana, ujezi ulisimama na kila mtu alitawanyika duniani kote. Mji ulikuwa ukiitwa _________________________ (mstari8) kwasababu _________________________________________________________
Kwa mara nyingine matokeo ya dhambi ni dhahiri. Dhambi husababisha kutengana na uharibifu wa mahusiano. Hebu tufanye marudio:
1. Tuliona jinsi dhambi ilivyosababisha matengano kati ya Mungu na mwanadamu na kati ya mume na mke katika Mwanzo 3.
2. Pia katika Mwanzo 3 tulijifunza kuwa dhambi ilileta laana katika ardhi, ardhi ambayo ilikuwa itoe chakula kwaajili ya binadamu.
3. Dhambi ilisababisha chuki katika familia kwa mfano halisi ni Kaini na Abeli.
4. Na sasa, tunaona kuwa dhambi imeleta mwisho wa kitu ambacho dunia ilikuwa bado inacho, _____________ lugha na _____________________ ulimi (Mwanzo 11:1).
Ili dunia iweze kujaa, Mungu alitaka watu watawanyike dunia nzima.

**Rejea Mungu alitaka nini…**

Mwanzo1:22
Mwanzo 1:27
Mwanzo 9:1

Mwanzo 9:19
Mwanzo 10:32
Mwanzo 11:8,9
**Rejea Mwanadamu alitaka nini…**
Mwanzo 11:4

**MATUMIZI:**

Uliisha shangaa na kutaka kujua ni wapi tofauti za lugha zilianzia ? Mawasiliano husabisha mchafuko mengi katika mahusiano hata tunapokuwa tukiongea lugha moja. Matumizi ya neno lisilosahii huleta vikwazo. Matumizi ya lugha za picha kuwasilisha maana fulani ambayo hujenga ukuta katikati. Mila na tamaduni hufanya lugha kuwa ngumu. Kama tukavyo endelea kuona katika Agano Jipya, katika kitabu cha Yohana, tunajifunza katika sura ya 1 kwamba, Yesu ni Neno, sehemu halisi ya mawasiliano ya Mungu. Anawasiliana neema na kweli (Yohana 1:14). Pasipo kujali maharibifu yote na ufisadi ambao dhambi ilisababisha. Yesu alikuja akiwa Neno la kweli la Mungu kuvunja mipaka yote ya dhambi na kutengeneza amani kati ya Mungu na mwanadamu na kati ya watu wote wa kila lugha na ulimi---wanaume na wanawake, weusi na weupe na kuumba amani kati ya Mungu na mwanadamu na kati ya watu wa kila kabila na ulimi ---wanaume ---wanawake, weupe, weusi, masikini, na tajiri na masikini, wadogo kwa wakubwa. Je unaweza kukumbuka ulipokutana na matatizo katika kuwasiliana na mwingine?

1. Ni nini kilicho sababisha matatizo?

______________________________________________________________________

2. Tatizo lilimalizikaje?

______________________________________________________________________

3. Majaribio yetu ya kuwasiliana mara nyingi hushindwa. Kukubali kushindwa kwetu na kuomba msamaha kwa mapungufu yetu ni tumaini la pekee la kuunganisha mahusiano yaliyo vunjika.
Uzoefu wako ni nini katika hali ya kurejesha mahusiano yaliyo vunjika?

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

**SALA:**

Tumia muda huu kuleta mbele ya Baba kukiri kwako binafsi, kwa kushindwa kuwasiliana vizuri na mwingine, labda hata ukiwa pamoja naye. Mshukuru kwa lugha ya upendo ambayo anatoa kupitia Yesu, Neno lililofanyika mwili (Yohana 1).

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

**SOMO LA IIX ~~SEHEMU YA 55**

Ukoo katika 11:10-32 inaweka msingi kwa ajili ya "habari yote inayobakia." Tumeona kizazi ambacho kimeunganisha Adamu na Nuhu. Tunafahamu kuwa Shemu ni mtoto wa pili wa Nuhu. Ni muhimu kupata picha kamili ili kufahamu uhusiano wa damu ambao unaunganisha Shemu na Abrahamu. Abrahamu ni babu ambaye Mungu alichagua na kumuita ili awe baba wa mataifa. Hebu tuanze na kipande cha mwisho

cha somo la 6 kwa kusoma habari ya ukoo katika Mwanzo 11:10-26. Angalia majina ambayo unafahamu kutoka sehemu ya 3.

**ZOEZI:**

**JinaUmri JinaUmri**
Shemu 500
Arfakisadi
Abram, Nahori,
Harani
Baadhi ya mambo ya kuzingatia…

- Linganisha urefu wa maisha au umri katika ukoo toka Adamu kwenda Nuhu katika sura ya 5.
- Majina kutoka Shemu hadi Pelegi yametajwa katika Mwanzo 10:21-25. Kilichotajwa katika mstari wa 25 inawezekana ikawa ni sababu ya tofauti ya majina kutoka kwa Pelegi hadi kwa Abramu?

**FUNDISHO:**

Maelezo zaidi yametolewa kuhusina na familia ya Tera, baba yake Abramu, Nahoro, na Harani.

- Harani alikuwa baba wa________________________________________ (mstari wa 27) Lutu alikuwa nani kwa Abrahamu
______________________________________________________.
- Nchi ambayoTera na wana wake walitoka iliitwa ______________________________________________________________________
- Mtoto wa Tera, baba yake Lutu __________________________________ alifariki (mstari 28).

89

• Abrahamu alioa
________________________________________________ na Nahori alioa
_______________________________________________________________
_

• Kuna uhusiano gani kati ya Milika na Nahori?
_______________________________________

• Milka pia alikuwa na dada yake
___________________________________ (mstari 29)

• Tunajifunza nini kuhusu mke wa Abramu Sarai katika mstari wa 30?
_______________________________________________________________
_________

Familia iko safarini. Hawa walikuwa ni wafugaji. Waliishi kwenye mahema walikuwa watu wa kwenda. Kama mkuu wa familia, au kiongozi wa kabila, Tera aliamua kuwa, ulikuwa ni wakati wa kuondoka.

• Waliondoka katika nchi ya
_____________________________________(mstari wa 31)

• Walikuwa kichwa kwa
___________________________________________________.

Hili ni neno lililo zoeleka tulilojifunza mwanzoni katia somo hili. Rejea sehemu ya 3 na ukoo wa Hamu, pia aliitwa Kanaani.

• Tera alikwenda na nani?
_______________________________________________________________
_________
_______________________________________________________________
_________

• Hawakuweza kufika Kanaani. Walifika na kuweka makazi wapi?
_______________________________________________________________
_________

• katika mstari wa 32, tunajifunza kwamba hapa ndipo mahali ambapo Tera alifariki. Aliishi miaka __________.

**MATUMIZI:**

Uliisha shuhudia kuhama kutoka sehemu moja ya nchi kwenda sehemu nyingine? Labda hapakuwa mbali, isipokuwa ulitoka sehemu ya eneo ulilozoea kwenda. Kumbuka uzoefu wako. Labda hukuwa na la kusema kuhusiana na tatizo, uliambiwa pakia vitu vyako…Mabadiliko yanaweza kuwa kutokuwa na maskani. Si kwamba hatutaki kumaliza matokeo isipokuwa hatua za kuchukua ili kumaliza matokeo hayo yanaweza kuleta machafuko na kusababisha machafuko. Kutokana na hisia ya kupata hasara, husababisha kuzuia mabadiliko ya kutoka sehemu moja na kwenda nchi ya mbali. Haufahamu uzoefu wa Abrahamu na Sarai walipoondoka na Tera kwa matazamio ya kwenda katika nchi ya Kanaani. Lakini walifunga mizigo yao wakaondoka pasipokufahamu yatakayotokea mbele zao. Rejea kuondoka ulikoisha fanya. Ni mambo gani yaliyo kusumbua zaidi kuhusiana na kuondoka kwako? Ni ni kilicho sababisha wasiwasi na mashaka?

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

Ni nani aliyefanya maamuzi ya kuondoka?

______________________________________________________________________

Ni aki na nani ulio ondoka nao?

______________________________________________________________________

Ulifanikiwa kufika kwenye kituo chako ulichokusudia, au mipango ilibadilika?

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

Kadiri tuavyoendelea kujifunza, tutaona juu ya mpango wa Mungu kwa ajili ya Abrahamu. Hakuna mashaka kwamba Abrahamu alitembea kwa imani, akisadiki kwamba Mungu alikuwa pamoja naye. Abramu anaondoka na mke wake, baba yake, na mjomba wake katika msafara wa kiufugaji kwenda kwenye nchi wasiyoifahamu. Wanaacha mazoea na kuanza tena katika nchi mpya. Tunafikia mwisho wa sura hii ya masomo na wako tayari kuacha hawa wasafiri wakiendelea na safari. Hadithi ya mpango wa Mungu kwaajili ya wanadamu inaanza. Katika sura inayofuata ya masomo tutarudia habari za Abramu na Sarai katika Mwanzo 12 na kujifunza ahadi kubwa za Mungu kama anavyo funua mipango yake kwao na uzao wao.

**SALA:**

Ee, Bwana Mungu wakati mwingine utatuita kuondoka japokuwa hatujui tuendako. Abramu alibalikiwa yeye na familia yake, ukoo wake, urithi uliokuwa chini ya uangalizi wa jicho lako

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

## MARUDIO

Hili sio JARIBIO! Wakati mwingine, pamoja na hayo, inatia moyo kuwa kutathimini kujifunza kwa mtu. Tunajiamini zaidi na kuhimizwa kuendelea mbele. Umemaliza masomo ya Biblia yenye kichwa kiitwacho *Mpango wa Mungu Chaguo Letu.* Hebu tukumbuke baadhi ya mambo uliyokuwa ukijifunza kwa majuma haya yaliyopita:

- Kuwa mzoefu na habari juu ya uumbaji katika Mwanzo

- Kujifunza juu ya Biblia isemavyo juu ya Mungu kama muumbaji
- Kuelezea kufafanua na kuelewa baadhi ya maneno:
  - Takasa
  - Siku ya Sabato
  - Kuhesabiwa haki
  - Neema
  - Ukombozi
  - Imani
  - Huruma
- Kutambua thamani ambayo Mugu huweka kwa binadamu kama walioumbwa kwa mfano wa Mungu
- Kufahamu wajibu wa binadamu kuonyesha mfano wake kwa uumbaji
- Kuelewa wajibu wa kuongezeka na kuujaza ulimwengu, kuutawala na kuutiisha
- Kujifunza mawazo ya Mungu juu ya ndoa
- Kutambua nia ya Mungu kwa binadamu kuishi na Neno lake kama kiini cha maisha ya mtu
- Kupanua ufahamu wako juu ya dhambi, tama zake, matokeo yake
- Kuwa na ufahamu juu ya Kaini na Abeli
- Kukua katika ufahamu juu ya hatari ya kuharibu uumbaji
- Kuwa na uelewa juu ya Nuhu na gharika
- Kujifunza ahadi ya Mungu kwa Nuhu na uumbaji wote
- Kufurahia thamani ambayo Mungu aliiweka juu ya uhai wa damu, sadaka, na maagano
- Kuwa na ufahamu juu ya uzao wa Nuhu
- Kujifunza juu ya uamzi wa Mungu wa kuvuruga lugha za wanadamu

Hongera! Umekamilisha masomo haya na umejifunza mengi. Lakini, kuna mengi ya kujifunza zaudu. Umemaliza somo la 6 – sehemu ya 6 kumalizia na ukoo wa Abramu katika Mwanzo 10. Abramu na mke wake Sarai, safari ya katika nchi ya Kanaani na baba yake Tera

aliyeamua kuishi Harani. Somo linalofuata litaanza na kuitwa kwa Abramu kuacha Harani na "nenda katika nchi nitakayo kuonyesha" (Mwanzo 12:1)

Kama mto unaotiririka ukiacha chanzo cha maji, ikichukua upana kutoka katika chemi chemi, utaongeza katika elimu yako na imani kama Mungu anavyotupa katika mto wa maisha.